# Nipashe

Jumanne Januari 9, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • Na. 0581550

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

UKURASA 21

## TEN HAG: KUNA WACHEZAJI HAWAMUDU PRESHA UNITED

**PM** akuta 'madudu' RUWASA, pikipiki mpya zaozea stoo, uchafu kwenye ofisi unatisha

UKURASA 2

**Mwanafunzi** aozwa kwa ng'ombe 15, DC wake amnusuru

UK.4



**Rais** Dk. Mwinyi ajivunia mageuzi elimu bila malipo

UKURASA 17

### MABORESHO SHERIA UCHAGUZI

# Taasisi, wadau waibua hoja 22

• **MAASKOFU** Katoliki walia na Mwenyekiti wa NEC; wanasheria TLS, LHRC nao wamo...*Endelea Ukurasa 2&3*

## Kenya yaiomba Tanzania msaada tiba kifua kikuu

UKURASA 19



Mwenyekiti wa Tume ya Huduma za Kijamii wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Askofu Yuda Thadaeus Ruwa'ichi, akiwasilisha maoni yao kuhusu miswada ya sheria ya uchaguzi kwa Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria bungeni, Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



## Mabasi yaliyopigwa 'stop' yaendelea kukatisha tiketi

• **DC:** Viongozi wakamatwe, RC Dar ateta nao ...*Ukurasa 4*

**MICHEZO** GAMONDI ATOA SABABU KIPIGO YANGA UK.23

**MAONI** UK.6



Bob Wangwe akitoa maoni yake katika mkutano wa wadau mbele ya Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TEC: Rais asiteue Mkurugenzi NEC

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA la Maaskofu wa Kanisa Katoliki (TEC) limependekeza Rais kuondolewa mamlaka ya kuteua Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ili kutokuwapo kwa mgongano wa kimaslahi wakati wa Uchaguzi Mkuu.

Mwenyekiti wa Tume ya Huduma za Kijamii wa Baraza hilo, Askofu Yuda Thadaeus Ruwa'ichi, alibainisha hayo jana alipowasilisha maoni ya TEC, kuhusu miswada minne ya sheria zinazohusu uchaguzi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwenye Ukumbi wa Msekwa, bungeni jijini hapa.

Alisema TEC inapendekeza kuondolewa mamlaka ya Rais kuteua Mkurugenzi wa NEC kwa kuwa uteuzi huo kufanywa na Mkuu wa Nchi, kunaleta mgongano wa kimaslahi.

Ruwa'ichi ambaye ni Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, alisema wanapendekeza Mkurugenzi wa NEC ateuliwe na chombo huru badala ya utaratibu wa sasa wa Rais kuteua na kuwaapisha mwenyewe.

"Tunapendekeza Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi kuteuliwa na chombo huru na kuapa kwa Jaji Mkuu au Jaji wa Mahakama ya Rufani badala kuapa kwa Rais," alisema.

Askofu Ruwa'ichi alisema kitendo cha Rais kumteua Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi na kuapa mbele yake kinachangia kuleta migongano ya kimaslahi na wakati mwingine kuharibu uchaguzi.

"Kitu hiki si sahihi kabisa, tunapendekeza Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi akiteuliwa, ateuliwe na chombo huru na kiapo afanye kwa Mwenyekiti wa Tume badala ya kuapa mbele ya Rais," alisema.

Vilevile, alisema ipo haja kwa Tume ya Uchaguzi kuacha matumizi ya watumishi wa umma kwenye Uchaguzi Mkuu kwa kuwa wamekuwa chanzo cha kuingilia michakato ya uchaguzi.

"Tume ya Uchaguzi waajiri watumishi wake nchi nzima ambao watatumika kuratibu shughuli za uchaguzi badala ya kuwatumia watumishi hawa kama vile wakurugenzi wa halmashauri au polisi ambao wamekuwa chanzo cha kuharibu mchakato wa uchaguzi," alisema.

Kadhalika, Askofu Ruwa'ichi alisema utaratibu wa kumpata Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi uondoe sharti la mtu ambye anachaguliwa kushika nafasi hiyo, lazima awe mtumishi wa umma.

"Watanzania wenye uwezo wapo wengi, lakini cha ajabu Mkurugenzi wa Tume lazima awe mtumishi wa umma. Hii inapaswa kubadilishwa ili kuwapo utaratibu wa watu wenye sifa kuomba kuteuliwa kushika nafasi hiyo," alisema.

Katibu wa TEC, Padri Dk. Charles Kitima, alisema hoja ya kuwapo Tume huru ya Uchaguzi ni jambo muhimu na linapaswa kufanyiwa kazi.

"Tume ya Taifa ya Uchaguzi lazima iwe ya wananchi na si kwa ajili ya wale wanaoitaka kwa maslahi yao. Tumetoa kwenye wasilisho letu mifano ya nchi ambazo zimefanya maboresho ya tume za uchaguzi hivi sasa hakuna shida kwa uchaguzi wa wabunge na madiwani, shida bado ipo kwa urais tu," alisema.

Miswada ambayo wadau wameitwa kutoa maoni bungeni ni ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023; Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa Mwaka 2023; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023.

cotex industries

TAARIFA KWA UMMA



OMARY ALLY MWINJUMA

Hii ni kutaarifu Umma kwamba mwenye picha hapo juu **OMARY ALLY MWINJUMA** si mfanyakazi tena wa **COTEX INDUSTRIES LTD** Mbezi Beach, Jogoo, Dar es salaam kuanzia tarehe 07.12.2023

Tunaomba kuutangazia Umma kwamba Kampuni ya **COTEX INDUSTRIES LTD** haitahusika na miamala itakayoingizwa au shughuli yoyote itakayofanywa na mtajwa hapo juu kwa jina la Kampuni.

**Utawala.**

# Ziara ya Waziri Mkuu yabaini shida RUWASA

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amemwagiza Waziri wa Maji, Jumaa Aweso kufika katika ofisi za Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Lindi na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi (LUWASA) kufuatilia upungufu uliopo ikiwamo kutotumika kwa gari la uchimbaji visima lililotolewa na serikali tangu Juni, mwaka jana ili kuwezesha uchimbaji visima vya maji.

"Hii wizara ina waziri makini sana, mnafanya vitu kwa kificho, sasa waziri aje hapa, mnamwona anavyohangaika waziri wenu, vitu vidogo vidogo hivi mpaka waziri aje na ninyi mpo? Kwanini mpo hapa?" Waziri Mkuu alisisitiza na kuongeza kuwa anahitaji taarifa ya kwanini mashine hiyo tangu imefika haijachimba kisima hata kimoja.

Alitoa maagizo hayo jana baada ya kufanya ziara katika ofisi za RUWASA zilizoko Manispaa ya Lindi na kushuhudia mtambo wa kuchimba visima ukiwa umeegeshwa na hakuna kisima kilichochimbwa tangu ulipotolewa mwaka jana huku katika mikoa mingine iliyopewa mtambo kama huo visima vinachimbwa kama ilivyokusudiwa.

Waziri Mkuu alihoji, "Ni kwanini mtambo huu haujaanza kufanya kazi kwa kipindi cha miezi sita ikiwa katika mikoa mingine imeshaanza kufanya hivyo.

"Mwezi wa sita (Juni) hadi leo (jana) hamjachimba hata kisima kimoja na mnasema kuna matope haiwezekani. Mheshimiwa Rais ameleta mtambo wananchi wameona gari limefika mnataka visima visichimbwe?"

Waziri Mkuu pia alihoji sababu ya kutotumika kwa pikipiki zilizonunuliwa na RUWASA Mkoa wa Lindi tangu mwaka 2021 kwa ajili ya kuzigawa kwa jumuiya za watumiaji maji kwa madai kuwa hazijapata usajili.

"Huu ni uzembe, haiwezekani fedha za wananchi zinapotea ninyi mpo tu. Hizi pikipiki zimeanza kuharibika," Majaliwa alisema.

Akizungumzia pikipiki hizo, Ofisa Ununuzi wa RUWASA Mkoa wa Lindi, Kenedy Mbagwa, alisema kwa muda mrefu wamekuwa wanafuatilia suala la vibali vya kutumia pikipiki hizo kutoka makao makuu ya RUWASA bila ya mafanikio.

Waziri Mkuu baada ya kupata maelezo hayo, alimwagiza Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi afuatilie suala hilo.

Majaliwa pia alieleza kuchukizwa na hali ya mazingira ya ofisi ya LUWASA ambayo haiendani na ofisi za umma, ni machafu na yana vichaka vingi.

"Hapa ndio ofisini? Kwahiyo, hapa tupo kazini?" Waziri Mkuu alihoji wakati akikagua maeneo hayo.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu ameagiza Wizara ya Maji na Msajili wa Hazina wafanye tathmini ya kina kuangalia utendaji kazi wa Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA) ambao umo ndani ya RUWASA kuona kama ipo haja ya taasisi hiyo kuendelea kujitegemea.

"Hamwezi kuwa na wakala wawili wanaofanya kazi moja kwenye taasisi moja," Waziri Mkuu alionya.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Lindi, Muhibu Lubasa alisema mkoa umejipanga kuanza kuchimba visima katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo kwa kutumia mtambo huo uliotolewa na serikali kuanzia mwezi ujao.

## SHERIA ZA UCHAGUZI

# TLS, LHRC, wadau waibuka na hoja 22

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa sheria na demokrasia wametoa mapendekezo 22 kuhusu miswada ya sheria zinazohusu uchaguzi, ikiwamo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iwe na mamlaka ya kuajiri watumishi wake kwenye ngazi zote.

Vilevile wadau hao wamependekeza matumizi ya teknolojia katika kufanya utambuzi wa wapigakura kwa njia mbalimbali ikiwamo dole gumba na tume ibainishe siku mahsusi ya uchaguzi, huku wakitaka jina la sheria ya uchaguzi ijulikane kama Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ambayo itatumika kusimamia uchaguzi wa ngazi zote na mambo yote yanayohusu uchaguzi nchini.

Wadau waliotoa maoni hayo ni Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Jukwaa la Katiba (JUKATA), Twaweza, CSL na Jamii Forum.

Katika uchambuzi wa miswada hiyo, wadau hao pia wanapendekeza watu waruhusiwe kupiga kura kwa vitambulisho mbadala vinavyotambulika kisheria.

Pia wanapendekeza kuwa endapo hadi siku ya mwisho ya uteuzi hapatakuwa na mgombea au mgombea amejitoa ndani ya saa 24 baada ya muda wa uteuzi kuisha, chama husika kipewe nafasi ya kuteua mgombea mwingine.

Katika maoni yao, wadau hao wanapendekeza mshindi wa nafasi ya urais, ubunge na madiwani apatikane kwa kura nyingi - zaidi ya nusu ya kura zote zilizopigwa, fomu ya uteuzi wa mgombea wa ubunge na udiwani na vifaa vya uchaguzi pamoja na miundombinu viandaliwe kwa kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Kadhalika, wanapendekeza usikilizwaji wa mashauri ya uchaguzi ukamilike ndani ya siku 90 badala ya miezi 12 kama inavyopendekezwa katika muswada husika na wakitaka rufani zikamilike ndani ya siku 60 badala ya miezi 12 kama inavyopendekezwa.

Pia wanashauri kuwekwe matakwa ya lazima kuwapo midahalo kwa ngazi ya urais na urushwe mubashara kwenye vyombo vya habari na kwa ngazi ya ubunge na kata midahalo hiyo ifanyike katika ngazi husika.

Mapendekezo mengine ni kuwapo kifungu kinachoainisha ukomo wa muda wa kutangaza matokeo ya urais, ubunge na madiwani, kuweka kifungu kitakachoweka wajibu kwa vyombo vya habari vya umma kutokuwa na upendeleo kwa kuwapa fursa sawa wagombea kujinadi na vyombo vya habari binafsi kuweka muda maalum kwa ajili ya wagombea wote wakati wa kampeni.



Baadhi ya wadau wakiwa katika ukumbi wa Msekwa Bungeni jijini Dodoma kutoa maoni yao kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu muswada wa Sheria na Katiba ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

Wanapendekeza kuwe na sura maalum kuhusu elimu ya mpigakura na watazamaji wa uchaguzi na uwasilishwaji fomu za uteuzi wa wagombea katika ngazi zote uwe kwa njia ya nakala ngumu au tepe.

Wadau hao wanapendekeza kuondoa kifungu cha 107(3) kinachopendekeza kuteketeza nyaraka za uchaguzi ndani ya miezi sita kwa kuwa kinakinzana na muda wa mashauri ya uchaguzi na Kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Taifa ya Utunzaji wa Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya Mwaka 2002 ambayo inaweka takwa la nyaraka za Taifa kutunzwa ndani ya miaka 30.

Mengine wanataka nyaraka za uchaguzi zitunzwe kielektroniki, kurekebisha kifungu cha 102(1)(e) kwa kuondoa maneno "iwapo fomu za taarifa za matokeo zipo za kutosha".

Wadau hao wa sheria na demokrasia pia wanapendekeza kwamba popote kwenye muswada huo palipoandikwa chini ya sheria pafutwe na pasomeke kwa mujibu wa sheria hii huku wakitaka popote penye neno tarehe iliyochaguliwa pafutwe na pasomeke tarehe iliyopangwa.

Mengine wanayopendekeza ni mtiririko wa vifungu vya muswada huo ufuate mzunguko wa kiuchaguzi ili kuleta mantiki na kurahisisha usomaji, uandikishaji, elimu ya mpigakura, uteuzi wa wagombea, kampeni, upigaji kura, matokeo, mashauri ya uchaguzi, kuondoa kifungu kinachoweka takwa la kutaifisha dhamana ya mgombea ikiwa hatopata moja ya kumi ya kura zote zilizohesabiwa.

Kesho ndiyo mwisho wa Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kupokea maoni kuhusu miswada hiyo.

Miswada hiyo ambayo wadau wameitwa kutoa maoni bungeni ni ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023; Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa Mwaka 2023; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023.

Miswada hiyo ilisomwa kwa mara ya kwanza bungeni Novemba 10, mwaka jana. Kuwasilishwa kwake kunatokana na kilio cha muda mrefu cha vyama vya siasa na wadau kuhusu uendeshaji wa uchaguzi nchini.


NANGE AUCTIONMART AND DEBT COLLECTORS LTD
P.O. Box 16284-ARUSHA (HQ), TEL. 0754 748323
MANYARA BRANCH
Dealers in: AUCTIONEERS, DEBT COLLECTORS COURTBROKERS, PROPERTY VALUERS AND COMMISSION AGENTS

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KWA WADAIWA WA MASHATI SACCOS**

Kwa idhini tuliyopewa na **Mashati saccos** tutauza kwa mnada wa hadhara mali za wadaiwa walioshindwa kulipa madeni yao

| S/N | JINA | DHAMANA | MAHALI ILIPO | TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MASHIMA SACCOS | SHAMBA | ROMBO-USERI | 24/1/2024 saa 9:00 Jioni Nakuendelea |
| 2 | PRISILA COSMAS KAVISHE | NYUMBA | ROMBO-MASHATI | 23/1/2024 saa 8:00 Mchana Nakuendelea |
| 3 | FELIX MARANDU | SHAMBA | ROMBO-MASHATI | 23/1/2024 saa 5:00 asubuhi Nakuendelea |
| 4 | VICTUS TEMU | SHAMBA | ROMBO MASHATI | 24/1/2024 saa 4:00 asubuhi Nakuendelea |
| 5 | JOACHM TESHA | NYUMBA | ROMBO-MASHATI | 24/1/2024 saa 6:00 Mchana Nakuendelea |
| 6 | CHARLES KAAYA | KIWANJA | BOMA NGOMBE | 27/1/2024 saa 4:00 asubuhi Nakuendelea |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei iliyofikiwa katika mnada, salio litalipwa ndani ya siku 14 toka tarehe yam nada huu
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mnada wa siku 14 atakuwa amepoteza haki yake mnada utarudiwa na 25% aliyolipa haitarudishwa
3. Wateja wataruhusiwa kukagua mali husika kabla ya mnada



**VISIT** FREE ENTRY
INTL TRADE EXHIBITION ON FOOD & PROCESSING PLASTICS & PACKAGING

EXHIBITORS FROM AROUND 13 COUNTRIES

**FOODPACK 2024**
INTL FOOD & PROCESSING TRADE SHOW - EAST AFRICA

**Products on Display:**
Juices | Refrigeration Systems | Storage Displays | Bakery Ingredients
Oil Seeds | Agro Commodities | Tea | Milk | Diapers | Rice

**INTERPLAST-PACK 2024**
INTL TRADE EXHIBITION ON PLASTICS, POLYMERS, RUBBER, CORRUGATED PACKAGING & PRINTING

**Products on Display:**
Paper | Disposable Packaging Machinery | Plastic Raw Material
Polypropylene | Woven Products

**Date & Venue**
26-28 January 2024
Diamond Jubilee Hall, Dar-Es-Salaam - Tanzania

**Timing**
10:00 AM TO 6:00 PM

For more info, Please Call
0768 616 418 / 0656 482 557



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (wa tatu kushoto), akiwa pamoja na baadhi ya wafanyakazi wa bomba la mafuta ghafi la Africa Mashariki (EACOP) baada ya kupokea msaada wa mifuko 1,000 ya saruji waliyoitoa kwa ajili ya waathirika wa maporomoko ya ardhi. Makabidhiano hayo yalifanyika wilayani Katesh jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabasi yaliyopigwa 'stop' yaendelea kukatisha tiketi

**Na Waandishi Wetu**

MAMIA ya abiria waliokuwa wanasafiri kutoka Moshi kwenda mikoa mbalimbali nchini kwa kutumia mabasi ya kampuni ya Kilimanjaro Express, wamekwama kusafiri katika ofisi za mabasi hayo mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro baada ya kampuni hiyo kufungiwa kutoa huduma na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA).

Nipashe ilishuhudia jana asubuhi adha hiyo baada ya LATRA kufungia kampuni hiyo juzi kutoa huduma ya usafiri kuanzia jana kutokana na makosa mbalimbali ikiwamo kutoza nauli kubwa kwa abiria, kutoa tiketi za kielektroniki na kuzidisha abiria.

Wakizungumza na Nipashe katika ofisi za mabasi hayo, baadhi ya abiria hao akiwamo Elisaria Assey, walisema kuwa walifika kituoni alfajiri kwa ajili ya kusafiri na magari ya kampuni hiyo, lakini hakukuwa na huduma.

Assey alisema kuwa walipofika katika ofisi za kampuni hizo walishangaa kuambiwa kuwa magari hayo yamefungiwa kutoa huduma, hivyo hawakujua hatima yao.

"Jana (juzi) nilifika hapa ofisi za Kilimanjaro Express na kukata tiketi kwa ajili ya kusafiri leo (jana) na walinitoza Sh. 50,000. Sasa nimejiandaa kwa safari, nimefika hapa tangu saa 11 alfajiri kwa ajili ya kusafiri, mpaka sasa ni saa tano asubuhi, bado nipo hapa na hatima yangu sijui ni ipi. Ninaomba serikali tusaidieni sisi tunaseka," alisema Welncesilaus Msuya.

Aliongeza: "Tangu asubuhi tumewaomba waturudishie nauli zetu tuweze kutafuta usafiri mwingine, wamekataa. Tuko hapa na hatujui hatima yetu ni nini."

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafi Ardhini (LATRA) Mkoa wa Kilimanjaro, Paul Nyello, alisema kuwa kuanzia Januari 8, mwaka huu, mabasi ya kampuni ya Kilimanjaro Express yamesimamishwa kutoa huduma ya usafiri kutokana na makosa mbalimbali.

Hata hivyo, Nyello alisema kuwa katika hali ya kushangaza, wamebaini mmiliki wa mabasi hayo amekaidi maagizo ya kusimamisha kutoa huduma ambapo mpaka jana asubuhi alikuwa anaendelea kupokea abiria na kukatisha tiketi.

"Tangu juzi tulitoa tangazo la kusitisha kusafirisha abiria kwa mabasi ya Kilimanjaro Express kuanzia leo (jana) mpaka pale watakapokidhi masharti ya usafiri, lakini cha kushangaza wameendelea kukaidi agizo kwani mpaka leo (jana) wameendelea kupokea abiria na kutoa tiketi kinyume cha taratibu.

"Hivyo, na sisi kama LATRA tutahakikisha hakuna gari la kampuni hii litakalotoa huduma," alisema Nyello.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kisare Makori, aliagiza LATRA kuhakikisha abiria wote waliokuwa wameshakatiwa tiketi katika mabasi ya kampuni ya Kilimanjaro Express wanasafari kama walivyopanga, huku hatua zingine za kisheria zikiendelea kufuata dhidi ya mmiliki wa mabasi hayo.

Makori alisema serikali kupitia LATRA ilisimamisha mabasi 35 ya kampuni hiyo kutoa huduma kutokana na kukiuka sheria iliyotungwa na Bunge ya kutaka kila kampuni ya mabasi inayotoa huduma ya usafirishaji abiria nchini kutoa tiketi za kielektroniki.

Alisema kosa lingine ambalo limekuwa linafanywa na kampuni hiyo ni kutoza nauli kubwa kulinganisha na bei elekezi ya LATRA; gharama halisi kutoka Moshi hadi Dar es Salaam ni Sh. 37,000, lakini kampuni hiyo imekuwa inatoza Sh. 44,000 hadi Sh. 55,000.

"Hiki kinachofanywa na kampuni ya Kilimanjaro Express ni wizi kama wizi mwingine. Haiwezekani abiria anatoka Moshi lakini anatozwa nauli ya abiria wa Arusha na wanakaidi maagizo ya serikali na kujiwekea utaratibu wao, hilo haliwezi kukubalika.

"Ninaagiza LATRA hakikisheni hawa abiria waliokuwa wasafiri kwa mabasi ya kampuni ya Kilimanjaro Express leo (jana) wanasafiri, watafutieni mabasi mengine wasafiri na hizo gharama zitalipwa na mmiliki wa Kilimanjaro Express," aliagiza.

Mkuu wa Wilaya pia aliagiza kukamatwa kwa watendaji wa kampuni hiyo ya mabasi na kuhojiwa kutokana na kilichotokea, ikizingatiwa tayari kulikuwa na zuio la mamlaka ya serikali iliyoyafungia mabasi yote ya kampuni hiyo.

**KIKAO DAR**

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Kilimanjaro Express, Roland Sawaya, jana alifanya kikao na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila na kumwomba azungumze na LATRA ili mabasi yake yaruhusiwe kutoa huduma ya usafirishaji.

Katika kikao hicho kilichohusisha Chalamila, LATRA na Jeshi la Polisi, mkurugenzi huyo alikiri kwamba amekuwa anapokea kesi nyingi zinazotokana na mabasi yake kulalamikiwa kusimamishwa barabarani.

"Nimemwomba Mkuu wa Mkoa aje asikilize hili jambo na asaidie kulitatua. Mimi nilikuwa ninataka siku nyingi kuongea na Mkuu wa LATRA na ninasukumwa sana kwa sababu hata huko njiani magari ya Kilimanjaro yanasimamishwa sana.

"Kwahiyo, unakuwa na wasiwasi kwamba kuna shida gani. Mkuu wa Mkoa ninaomba msaada wako na biashara yangu isipofunguliwa itakuwa imekufa kabisa," alilalama Sawaya.

Baada ya maelezo hayo, Chalamila alimtaka atekeleze masharti yote aliyoambiwa na LATRA ili magari yake yafunguliwe.

Chalamila alisema: "Kufungua biashara kumeruhusiwa kabisa, lakini kwa masharti ambayo umepewa. Kwahiyo, wewe fanya hayo na mabasi yako yatafunguliwa na kama una madeni makubwa umalize na ukileta ujanjaujanja utafungiwa milango."

***Imeandaliwa na Mary Mosha (MOSHI), Elizabeth Zaya (DAR)**

## Mwanafunzi anasurika kuozwa mahari ya ng'ombe 15

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWANAFUNZI wa kidato cha kwanza mkazi wa Kijiji cha Iyugi, Kata ya Lyamidati wilayani Shinyanga, amenusurika kuozwa ndoa ya utotoni kwa mahari ya ng'ombe 15.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, wakati wa ziara yake ya kukagua mahudhurio ya wanafunzi ambao wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, pamoja na uandikishaji wa wanafunzi wa awali na darasa la kwanza katika shule mbalimbali ikiwamo Shule ya Sekondari ya Wasichana.

Akiwa katika shule hiyo iliyopo Butengwa, Manispaa ya Shinyanga, alisema amesikitishwa na kitendo cha mzazi mmoja (jina lake limehifadhiwa) kutaka kukatisha ndoto za mtoto wake kwa tamaa ya kupata mahari ya ng'ombe 15 na kuamua kumwozesha.

"Mwanafunzi huyu jina lake tumelihifadhi amepata ufaulu daraja 'A' lakini cha kusikitisha baba yake mzazi hataki asome na kuamua kutaka kumwozesha kwa mahari ya ng'ombe 15, lakini ndoa hiyo haikufanikiwa ili tibuliwa na mwanafunzi kwa sasa yupo shuleni akiendelea na masomo yake ya kidato cha kwanza," alisema Mndeme.

Alisema kuwa baba mzazi wa mwanafunzi huyo wanamtafuta kutokana na kukimbia kusikojulikana baada ya kusikia akitafutwa na vyombo vya dola.

Aidha, Mndeme alitoa wito kwa wazazi na walezi mkoani humo kuacha tabia ya kuozesha wanafunzi ndoa za utotoni na kutaka wawaache wasome ili watimize ndoto zao za kuwa viongozi wa baadae wa taifa.

Nao baadhi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaosoma shule ya Sekondari ya Wasichana Shinyanga, walitoa wito kwa wazazi wasiwabague watoto wa kike katika elimu, watoto wote wa kiume na kike wana haki sawa ya kupata elimu na kuziishi ndoto zao.

Mkuu wa sekondari hiyo, Nurah Kamutu, alisema shule hiyo imepangiwa wanafunzi wa kidato cha kwanza 143, lakini mpaka sasa wameshariporti wanafunzi 10.

HABARI KITAIFA

# 'Master plan' ya miundombinu nchini mbioni

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema inaandaa mpango mkuu wa miundombinu ya nchi kulingana na mahitaji ya kiuchumi na kijamii itakayowezesha kurahisisha usafiri na usafirishaji kulingana na ongezeko la watu nchini.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa alitoa taarifa hiyo jana alipokutana na Waziri wa Ardhi, Miundombinu, Usafiri na Utalii kutoka Japan, Konosuke Kokuba ambaye ameongozana na wataalamu mbalimbali wa sekta ya ujenzi nchini humo.

Waziri Bashungwa alisema mpango huo utaangazia mtandao wa barabara wa nchi nzima kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

"Miundombinu ya barabara inaenda sambamba na miundombinu mingine kama vile reli, kwa hivyo tutashirikiana na Wizara ya Uchukuzi kuandaa master plan (mpango mkuu) wa miundombinu katika kuhudumia Watanzania," alisema Waziri Bashungwa.

Aliielekeza TANROADS kuandaa majadiliano ya washauri elekezi na makandarasi kutoka Tanzania na Japan ambao utakuwa endelevu ili kuendeleza ushirikiano wa karibu katika sekta hiyo.

Aidha, Waziri Bashungwa alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameshatoa maelekezo mahsusi ya kuweka mazingira wezeshi kwa makandarasi wazawa na Wizara ya Ujenzi imeanza kupitia mpango wa ununuzi ambao awali ulikuwa unawabana makandarasi hao.

Waziri Bashungwa alipongeza Serikali ya Japan kwa ushirikiano wanaoendelea kutoa tangu Tanzania ilipopata uhuru na kuzialika sekta binafsi kutoka nchi hiyo kufanya kazi na kampuni za Tanzania kwa ukaribu zaidi ili kubadilishana uzoefu.

Aidha, ujio wa waziri huyo umekuja muda sahihi kwa kuwa serikali inakwenda kuboresha Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), kama mdau mkubwa wa matengenezo ya magari aina ya TOYOTA ambayo kwa asilimia kubwa yanatumika serikalini na kuhitaji msaada wa kiufundi.

Kokuba alisema kuwa serikali ya Japan itaendelea kuimarisha uhusiano kati ya nchi hizo kwa kuendelea kujenga miundombinu yenye ubora katika miradi yote inayoendelea na ile ambayo inatarajiwa kutekelezwa.

Alisema ongezeko la watu katika nchi zinazokuwa zinahitaji teknolojia za kisasa katika ujenzi wa miundombinu nchini ili ziweze kutosheleza mahitaji.

Mkutano huo umezikutanisha taasisi za wakala wa barabara TEMESA), Wakala wa Majengo (TBA) na Jumuiya ya Maendeleo ya Miundombinu ya Japani - Afrika (JAIDA).



Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Thomas Apson (kulia), akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Mwankhalaja, Kata ya Mgungira, wilayani humo mkoani Singida ambao nyumba zao 22 zimebomoka kutokana na mvua inayoendelea kunyesha na kusababisha mafuriko. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wizara ya Ardhi yaboresha mfumo unganishi Arusha

**Na Munir Shemweta,**
ARUSHA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Utalii imeipongeza Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kufanya kazi ya maboresho ya mfumo unganishi wa usimamizi wa sekta ya ardhi inayofanywa na timu ya wataalamu mkoani Arusha.

Akizungumza baada ya hitimisho la wasilisho la kazi ya uboreshaji mfumo huo, Mwenyekiti wa Kamati, Timotheo Mzava, aliipongeza Wizara ya Ardhi kwa kazi kubwa na nzuri ambayo inakwenda kuacha alama kwa Rais Samia Suluhu Hassan katika kipindi chake cha uongozi kwa kuicha sekta ya ardhi katika mifumo bora.

"Nichukue fursa hii kumpongeza Rais kwa kazi hii nzuri, kama kamati wameridhishwa na kazi na hongereni sana na mfumo huu uende ukawe bora na kutoa huduma kwa Watanzania," alisema Mzava.

Baadhi ya wabunge walisema mfumo huo sio tu utarahisisha na kuharakisha huduma za sekta ya ardhi bali utajibu maswali mengi yakiwamo ya kijamii.

"Niipongeze Wizara ya Ardhi kwa kufanyia kazi mfumo utakaojibu maswali mengi ya kijamii na ningetamani mfumo huu ungejibu maswali na changamoto za kiuchumi," alisema Lucy Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum.

Mbunge Makete mkoani Njombe, Festo Sanga, alisema kuwa uboreshaji huo umechelewa ingawa uko katika hatua nzuri. Hata hivyo, alitaka kufahamu utayari wa Wizara ya Ardhi katika kutumia mfumo husika kwenye eneo la usalama wa mifumo.

Aidha, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini, Emanuel Adamson alitaka kufahamu uimara wa utekelezaji mfumo huo kwa kuwa kumekuwa na mifumo mingi, lakini wakati wa utekelezaji kuwa na changamoto ikiwamo kuelezwa mtandao uko chini.

Mfumo huo unganishi wa usimamizi wa sekta ya ardhi unatarajiwa kuanza katika mikoa mitano ya Arusha, Dodoma, Mwanza, Mbeya na Tanga na utarahisisha na kuharakisha upatikanaji huduma za sekta ya ardhi kwa kuwa wananchi watakuwa wakipata huduma kwa njia ya mtandao.

# Serikali kuwalipa fidia watakaopisha Hifadhi Serengeti

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI inatarajia kulipa fidia ya zaidi ya Sh. bilioni 59 kwa wakazi wa Kata ya Nyatwali Bunda, mkoani Mara, kupisha eneo hilo, kwa ajili ya ikolojia viumbe hai vya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, alipotembelea eneo hilo mwishoni mwa wiki na kuzungumza na wakazi wa Nyatwali, katika mkutano wa hadhara mwishoni mwa wiki.

Aliwataka wakazi hao kuwa na subira na kuendelea na shughuli za kilimo na uzalishaji mali, huku serikali ikifanya ufuatiliaji wa jambo hilo na kwamba haitawaondoa eneo hilo bila kulipa fidia.

"Zoezi la uthamini lilishakamilika na kupelekwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali ambapo Shilingi zaidi ya bilioni 59 zinahitajika kulipa fidia kwa wananchi 4,111 waliofanyiwa uthamini na kujaza fomu namba 69 ambayo ni ya kukubali kufanyiwa uthamini," alisema Mtanda.

Mtanda alisema hajaenda eneo hilo kwa lengo la kuwatangazia wahame, bali kuwaondoa hofu na kuwataka kuwa na subira wakati utaratibu wa kuandaa fidia ukiendelea.

Alisema wanaolima waendelee na kilimo katika mashamba yao na serikali haiwezi kukata mazao ya mwananchi na kwamba serikali haiwezi kuruhusu wapate shida.

"Lakini pia tuache upotoshaji kwenye jambo hili kwamba hakuna fidia, wakati ukifika, kila mtu atalipwa haki yake ili kupisha ikolojia viumbe hai vya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti," alisema.

Pia serikali inafanya jitihada ili kila mwananchi wa Nyatwali apate haki yake inayostahili, kipindi hiki ambacho inaendelea na utaratibu wa kuandaa fidia, wananchi na waendelee na shughuli zao na pia wanafunzi wapelekwe shule.

Awali, Mbunge wa Bunda Mjini, Robert Maboto, alimwomba Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya Bunda, kuungana na watafute njia ya kumwona Rais Samia Suluhu Hassan kumweleza changamoto za Nyatwali.

Maboto alisema, kumekuwa na utata wa fidia kuhusu uhamaji wa wakazi wa kata hiyo, njia nzuri ni yeye (mbunge), mkuu wa wilaya na mkuu wa mkoa kwenda kwa Rais kupata ufafanuzi.

"Ni muda mrefu wananchi hawajalipwa fedha zao wakati tayari wameshafanyiwa tathmini ya mali zao, hivyo ninaomba wewe na mkuu wa wilaya twenda kwa Rais kupata ufafanuzi," alisema Maboto.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wazazi/walezi acheni kupuuza usalama wa watoto wenu

**WAKATI** kikikaribia kipindi cha kufungua shule, Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani lilionya watoto walio chini ya umri wa miaka tisa kupakiwa kwenye usafiri wa bodaboda ili kuepuka ajali zinazoweza kuwapata watoto hao.

Baadhi ya wazazi/walezi wamezoea kutumia usafiri huo kwa kuwarahisishia watoto wao wanapokwenda shule na kurudi nyumbani kutembea umbali mrefu.

Ni kweli usafiri huo umesaidia kwa kiasi kikubwa kuwapunguzia watoto mwendo kwa kuwa wanapofika shule huwa wamechoka na kushindwa kuzingatia masomo kwa umakini.

Vile vile, wakati wanaporudi nyumbani hutumia muda mwingi kucheza njiani na wanapofika hata kujisomea wanashindwa kwa sababu wanakuwa wamechoka sana.

Pamoja na usafiri huo kurahisisha safari, lakini hatari kubwa huwakabili watoto wao kwa kuzingatia wanavyopakiwa kwenye bodaboda hizo.

Kwanza bodoboda hazina kofia ngumu kwa ajili ya watoto na madereva wa usafiri huo hupendelea kuwaweka watoto mbele ya kiti chao huku upepo ukiwapiga na wanakuwa hawajavaa majaketi ya kuwakinga na upepo huo.

Kitendo cha madereva wa bodaboda kuwapakia watoto hao kwa mtindo wa mishikaki ni cha hatari kwa sababu inapotokea ajali ya kukanyaga kitu chochote kigumu na pikipiki kuruka, watoto wote wanaweza kuanguka na kusababisha balaa kubwa.

Madereva wengi wa bodaboda ni wale waliojifunza vijiweni na kuingia barabarani kupakia abiria bila kujua sheria za barabarani.

Vifo vingi vinavyosababishwa na madereva wa bodaboda ni vya kizembe ambavyo hufanyika kwa kujifanya wanajua kucheza na barabara kwa kupenya kwenye magari katikati bila kujali wamepakia viumbe ambavyo vinategemewa na wazazi na taifa kuwa viongozi wajao.

Katika kipindi cha kati ya Julai 2021 hadi Machi 2022, Bunge lilielezwa kuwa Tanzania kulikuwa na jumla ya matukio 1,594 ya ajali za barabarani na kati ya hizo 300 zilisababishwa na madereva wa bodaboda.

Daktari mmoja bingwa wa mifupa na viungo kutoka hospitali ya MOI, aliwahi kusema kuwa tatizo la ajali za bodaboda limekuwa likiongeza Tanzania tagu usafiri huo uanze kuingia nchini miaka ya 2009. Inaelezwa kuwa kuna siku hospitali hupokea wagonjwa watano mpaka kumi na wastani wa wagonjwa watano hadi sita kwa siku ni wa bodaboda.

Ikilinganishwa na majeruhi wanaopokewa wa bodaboda na wanaopokewa wa ajali zingine, inaonekaa bado wa bodaboda ni wengi kuliko wa magari.

Takwimu hizi zinatukumbusha kuwa usafiri wa bodaboda si salama sana kwa watoto hata watu wazima kutokana na ajali zinazotokana na usafiri huo.


Athari zinazotokana na ajali hizo ni vifo na kupata ulemavu wa kudumu ambao humrudisha mtu nyuma kimaendeleo na kushindwa kujitafutia riziki.

Watoto ambao ni tegemeo la baadaye hukwamishwa ndoto zao kwa kusababishiwa ajali na kupoteza maisha au kupata ulemavu wa maisha.

Jukumu la wazazi ni kuhakikisha watoto wao wanakuwa salama kwa kuwatafutia usafiri ulio salama kwao. Ni bora kutumia gharama kubwa ya usafiri kuliko kumweka mtoto kwenye hatari hiyo ya usafiri wa bodaboda.

Cha msingi ni kuzingatia maelekezo yanayotolewa na kikosi cha usalama barabarani ili kuokoa maisha ya watoto hao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kurudia mitihani ni kubembeleza wezi

Na Sabato Kasika

**KUENDELEA** kuwapangia tarehe za kurudia mitihani baada ya kufanya udanganyifu iwe darasa la nne, la saba au sekondari kunaweza kufananishwa na kulea na kubembeleza wezi wa mitihani na wachafu wa elimu.

Ni kwa sababu kufanya udanganyifu, lakini pia wanafunzi wengine kuandika matusi badala ya majibu ya mitihani kunajirudia kila mwaka na sasa kwenye matokeo ya mtihani wa darasa la nne na kidato cha pili yanayotangazwa mwishoni mwa wiki.

Huu siyo wakati wa kuendelea kufuta mitihani na kuwapangia waliodanganya tarehe ya kuurudia badala yake ni kuwashitaki na kuwafungia moja kwa moja na ili liwe funzo kwa wahusika.

Udanganyifu wa mitihani unajirudia kila mwaka, licha ya kwamba maonyo hutolewa mara kwa mara kabla ya wanafunzi kufanya mitihani hiyo, kitendo ambacho kinaonyesha kuwa kimekomaa.

Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), limetangaza matokeo ya mtihani wa darasa na nne na kidato cha pili uliofanyika mwaka jana, huku wanafunzi 206 wakifutiwa matokeo yote.

Wamefutiwa kwa kubainika kuwa wamefanya udanganyifu, lakini pia wanafunzi wengine 17 kwa kuandika matusi.

Bila kuchukua hatua kali zaidi, udanganyifu katika mitihani unaanza kuonekana kama jambo la kawaida, lakini madhara yake ni makubwa ikiwamo kupata wasomi mbumbumbu au vihiyo.

Kwa mfano, mwaka juzi wanafunzi 2,194 kati ya watahiniwa 1,350,881 waliofanya mitihani walifutiwa baada ya kubainika kufanya udanganyifu.

Ufutaji wa matokeo yawe ya sekondari na elimu ya msingi ni matukio ya kila mwaka ambayo ni vyema yangetafutiwa ufumbuzi wa kudumu kwa kudhibiti mianya yote inayosababisha kuwapo kwa vitendo hivyo.

Ninaamini udanganyifu wa mitihani ukidhibitiwa elimu itaokolewa, kwani mtondo huo umekuwa ukiporomosha elimu, hivyo ni vyema uchunguzi wa kina ufanyike kubaini chanzo cha udanganyifu huo.

Inawezekana baadhi ya wanafunzi wanakuwa na ufaulu wa juu na kuchaguliwa kwenda shule za vipaji, lakini kumbe umetokana na udanganyifu, hivyo hawezi kuwa na uwezo darasani.

Ni vyema kutambua kuwa udanganyifu wakati wa mitihani na wizi wa mitihani, vina athari kwa mtu mmoja kwa mwanafunzi, mwalimu, shule na taifa kwa ujumla, hivyo mtindo huo ungekomeshwa.

Kama kuna baadhi ya maafisa elimu wanaoshirikiana na walimu kujihusisha na wizi, udanganyifu na uvujaji wa mitihani waache mtindo huo, kwani unaharibu elimu na unashusha heshima na hadhi nchi.

Vilevile, ni wakati wa kukijua chanzo cha mchezo huo mchafu, kutafakari na kuchunguza kwa kina, nini chimbuko na athari za kuvuja kwa mitihani na nini kifanyike kwa lengo la kudhibiti vitendo hivyo.

Haitoshi kufuta matokeo na kisha kupanga tarehe nyingine ya kuruudia, huku mchezo ukiendelea kujirudia kila mwaka kana kwamba wahusika wameshindwa kudhibitiwa.

Sidhani wanafunzi wanahusika moja kwa moja katika udanganyifu huo, ndiyo maana hufutiwa matokeo na kupangiwa tarehe nyingine ya kufanya mitihani si tiba ya tatizo, lakini si vibaya wakasaidia kujua chanzo cha udanganyifu huo.

Shule zinapopambana au kushindana katika kufaulisha wanafunzi ni jambo jema, lakini zisifaulishe kwa njia ya udanganyifu kwa lengo la kuvutia wazazi na walezi ili wapeleke watoto wao huko.

Biashara ya ufaulu kwa njia ya udanganyifu zinazotumiwa kama nyenzo au ngazi ya kumvukisha mwanafunzi kutoka daraja moja hadi lingine, kimasomo bila kujali ufahamu au uelewa wake ni tatizo.

Kuendelea kwa biashara hiyo ni sawa na kuichimbia kaburi elimu na taaluma ya wanafunzi ambayo mwisho wake ni kubaki na taifa la watu wenye ukosefu wa fikra, weledi, ujuzi na ufahamu.

Hivyo, ingependeza kama NECTA wataweka mikakati mingine zaidi ambayo itakuja na matokeo chanya badala ya kuingia mitandaoni na kutoa maonyo makali ambayo mwisho yake hayatekelezwi.

Mitihani hiyo isiwe sehemu ya baadhi ya watu kufanya udanganyifu kwa ajili ya kupata maslahi binafsi na kuchangia kuporomosha elimu, bali iwe na kwa manufaa ya maendeleo ya elimu.

# Waziri aagiza TANROADS kurejesha mawasiliano barabara Rukwa-Songwe

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya, ameagiza Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) kuhakikisha unafungua mawasiliano ya barabara kutoka Katavi kwenda Songwe kupitia Bonde la Mto Rukwa.

Kasekenya aliagiza hayo jana wakati akikagua daraja hilo ambalo limeathiriwa na mvua inayoendelea kunyesha na hivyo kusababisha kukatika kwa mawasiliano kati ya mikoa hiyo.

"Niwaagize TANROADS kuhakikisha kazi inaendelea bila kusimama na mawasiliano yanarudi kama ilivyokuwa hapo awali, maana daraja hili ni muhimu kwa wananchi wa Kata ya Mto Wisa na Kata ya Zimba, pia mikoa ya Rukwa na Songwe kwa ujumla," alieleza Kasekenya.

Naibi Waziri pia alitoa rai kwa wananchi kuendelea kutunza miundombinu ya barabara ili iendelee kutumika na kuacha kufanya kazi kwenye vyanzo vya maji kwa kuwa barabara ni za wananchi wenyewe na si za serikali.

Pia aliitaka TANROADS na Bodi ya Mfuko wa Barabara kuhakikisha wanazitembelea barabara mara kwa mara katika kipindi hiki cha mvua ya El-Nino.

"TANROADS na Road Fund (Mfuko wa Barabara) kuna haja kupita kwenye haya maeneo ya barabara na madaraja kupata tathmini ya mahitaji na changamoto ili wanapokuja kuomba fedha za dharura wapewe kukabiliana na changamoto zinazojitokeza kwa haraka," aliagiza.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Rukwa, Mgeni Mwanga, alisema tayari timu ya wataalamu kutoka sehemu mbalimbali wameshafika na wanahakikisha wanafanya kazi usiku na mchana ili kurudisha mawasiliano ya barabara katika daraja hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Nyakia Ally, alisema mvua kubwa iliyonyesha imesababisha madhara kwenye mashamba, nyumba, barabara na madaraja na wanashukuru TANROADS kwa kuanza kazi ya kurejesha daraja lililokatika.

"Tunashukuru serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na TANROADS kwa kutujengea daraja la muda tukiwa tunasubiria kurejeshewa kwa daraja la awali ambalo mawasiliano yake yamekatika," alisema Nyakia.

Kurejeshwa kwa daraja la Mto Rukwa ambalo linaunganisha mikoa ya Rukwa, Katavi na Songwe, kutaimarisha uchumi, biashara na uwekezaji wa wananchi katika mikoa hiyo.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma (mwenye ushungi mwekundu), akiweka jiwe la msingi la Shule ya Msingi ya Kidichi ikiwa ni shamrashamra za Miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Mndeme aonya wazazi, walezi wanaoficha watoto wenye ulemavu

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amewataka wazazi na walezi mkoani mwake kutoficha watoto wenye ulemavu, bali wawapeleke shuleni ili wapate haki ya elimu na kutimiza ndoto zao.

Aliagiza hayo jana alipotembelea baadhi ya shule mkoani mwake kuangalia mahudhurio ya wanafunzi katika kuanza mwaka mpya wa masomo wa 2024.

Mkuu wa Mkoa alisema wazazi na walezi wanapaswa kuwapeleka watoto wao kuanza safari ya elimu, wakiwamo wenye ulemavu na si kuwaficha ndani.

"Serikali tumeboresha miundombinu ya shule ambayo sasa ni rafiki pia kwa wanafunzi wenye ulemavu.

Pia elimu inatolewa bure. Ninawasihi wazazi wapatieni elimu watoto ili wasome na kutimiza ndoto zao na baadaye waje kuwa viongozi wa taifa hili," alisema.

Mkuu wa Mkoa alisema serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya shule kwa kujenga vyumba vipya vya madarasa na sasa wameshajenga vyumba vipya 603 ili wanafunzi wasome katika mazingira rafiki.

Pia aliwataka walimu waendelee kufundisha kwa bidii ili wanafunzi wapate kuelewa masomo, akisisitiza ni lazima kila mtoto ajue kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwenge ambayo ni miongoni mwa shule zilizotembelewa na Mkuu wa Mkoa, Hassan Hemed, alitaja idadi ya wanafunzi ambao wameshaandikisha darasa la awali kuwa ni 80 kati ya wanafunzi 156 na kwa darasa la kwanza, wameandikisha wanafunzi 217 kati ya wanafunzi 230 wanaopaswa kuandikishwa mwaka huu. Mkuu wa Shule ya Sekondari Ngokolo, James Msimbe, alisema mpaka jana walikuwa wameshapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza 79 kati ya 347. Wanaendelea kupokea wanafunzi.

Katika ziara hiyo ya Mkuu wa Mkoa mbali na kutembelea shule hizo, pia aligawa madaftari na kalamu kwa wanafunzi katika shule zote ambazo alitembelea kukagua kuripoti kwa wanafunzi.

# Upelelezi wakwamisha kesi inayomkabili wakili

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa Mashtaka umedai mahakamani kuwa upelelezi wa kesi ya kuongoza genge la uhalifu na kusababisha hasara ya Sh. 2,161,705,744.50 kwa Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) inayomkabili Wakili wa Kujitegemea Henry Kishaluli (51), haujakamilika.

Wakili huyo anashtakiwa kwa makosa manne katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam ambayo ni kughushi, kuwasilisha nyaraka ya uongo, kuongoza genge la uhalifu na kusababisha hasara ya zaidi ya Sh. bilioni mbili.

Wakili wa Serikali Frank Michael alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Aron Lyamuya kuwa kesi iliyletwa kwa ajili ya kutajwa na upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Baada ya Wakili Michael kudai hayo, Hakimu Lyamuya aliahirisha kesi hiyo hadi Januari 23, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia.

Ilidaiwa kuwa kati ya Oktoba Mosi, 2011 na Machi Mosi, 2014, katika Mkoa wa Dar es Salaam, mshtakiwa, akishirikiana na wenzake tisa, kwa makusudi waliongoza genge la uhalifu kisha kusababisha hasara ya Sh. 2,161,705,744.50 kwa TGFA.

Katika shtaka la kughushi, inadaiwa mshtakiwa Mei 28, 2013 mkoani Dar es Salaam, alighushi barua ya kumiliki akaunti ya benki yenye jina la Karim Guram Hussein katika benki ya Habib African Bank yenye tarehe Mei, 28, 2013 ikionesha barua hiyo imeandikwa na kutiwa saini na Karim Guram Hussein jambo ambalo si kweli na ni kinyume cha sheria. Inadaiwa kuwa Juni 3, 2013, katika benki ya Habib African Bank wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa aliwasilisha nyaraka hiyo kwa Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo. Mashtaka mengine yanayomkabili Kishauli ni kusababishia TGFA hasara ambapo kati ya Oktoba Mosi, 2011 na Machi 31, 2014, yeye na wenzake tisa kwa vitendo vyao waliusababishia wakala huo hasara ya Sh. 2,161,705,744.50.

# KINANA ASEMA...

# Hakuna sababu kumnyima Rais Samia kipindi cha pili

## -Majaliwa ataja makubwa miaka mitatu madarakani

**Na Mwandishi Wetu,**
RUANGWA

ILI kiongozi yeyote afanikiwe kutimiza wajibu na dhamira ya kuwatumikia wananchi wake na kuwaletea maendeleo, ni lazima awe na watendaji au wasaidizi walio tayari kutekeleza majukumu yao wakati wowote na kwa kuzingatia weledi na uaminifu.

Dhamira hiyo ndiyo inayoelezwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa katika kuhakikisha anamsaidia kikamilifu Rais Samia Suluhu Hassan ili malengo yake ya kuwaletea maendeleo Watanzania na nchi kwa ujumla yafanikiwe kwa asilimia 100.

"Wananchi wa Ruangwa tutafanya kazi usiku na mchana, wakati wa jua kali na wakati wa mvua kali kuhakikisha tunamsaidia Mheshimiwa Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan ili atekeleze yale ambayo amepanga kuyafanya kwa Watanzania," alisema.

Waziri Mkuu alitoa kauli hiyo Januari 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Likangara, wilayani Ruangwa, alipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Jimbo la Rangwa, mkoani Lindi kwa kipindi cha miaka mitatu (2020-2023).

Majaliwa aliwasilisha taarifa hiyo katika Mkutano Mkuu Maalum wa CCM Wilaya ya Ruangwa ambapo mgeni rasmi alikuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana. Mkutano huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa CCM.

Waziri Mkuu alisema Rais Samia ameliwezesha taifa kuendelea kuwa na utulivu, maelewano na mshikamano, hivyo kuwawezesha wananchi kuendelea kushiriki ipasavyo katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Majaliwa alitumia fursa hiyo kuishauri Kamati Kuu ya CCM (CC) na Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) kutoa fomu moja kwa nafasi ya urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 na fomu hiyo iwe ya Rais Samia.

Waziri Mkuu alitoa ushauri huo kutokana na kile alichotaja kuwa ni uongozi bora na utekelezaji ilani unaofanywa kwa vitendo na Rais Samia ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Taifa.

Alisema kuwa Rais mbali na kutekeleza ilani kwa vitendo, pia ameendelea kuwatumikia Watanzania na kuwaletea maendeleo bila ya ubaguzi wowote.

Alisema kwa upande wa wananchi wa Ruangwa, wamejipambanua kwa kuishukuru serikali kwa vitendo kwa kufanya kazi kwa bidii na maarifa kuhakikisha Ilani ya Uchaguzi ya CCM inaendelea kutekelezewa kama ilivyokusudiwa.



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Abdulrahman Kinana, akisalimiana na wanachama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**MAMBO MAKUBWA**

Waziri Mkuu alitaja baadhi ya masuala makubwa ya kitaifa yaliyofanywa na Rais Samia tangu alipoingia madarakani ikiwamo kuendeleza miradi ya kielelezo na ya kimkakati ukiwamo ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa Reli ya Kiwango cha Kimataifa (SGR) na madaraja makubwa.

Kwa upande wa Wilaya ya Ruangwa, Waziri Mkuu Majaliwa alitaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana tangu Rais Samia aingie madarakani ni pamoja na uboreshwaji huduma za kijamii zikiwamo za afya, elimu, maji, miundombinu ya barabara na kilimo, hivyo kuwawezesha wananchi kupata maendeleo.

Akizungumzia huduma za afya, Waziri Mkuu alisema serikali imewezesha ujenzi wa hospitali ya wilaya; ujenzi wa vituo vya afya vipya vinne katika kata za Malolo, Nangurugai, Narungombe na Namichiga; ujenzi wa zahanati mpya tisa za Namungo, Mbangara, Muhuru, Namkatila, Mkaranga, Mihewe, Lipande, Mkutingome na Mtakuja na hivyo kuwezesha wananchi kupata huduma karibu na makazi yao na kwa wakati.

Majaliwa alisema kuwa mbali na uboreshaji mkubwa uliofanyika katika sekta za afya na elimu, pia imefanyika hivyo katika miundombinu ya usafiri na usafirishaji ambapo kwa sasa wilaya inaendelea na ujenzi wa barabara ya Nanganga-Ruangwa yenye urefu wa kilometa 56. Aliitaja ni barabara ambayo ni mhimili na mkombozi kwa shughuli za kiuchumi kwa Ruangwa.

Pia alisema wilaya hiyo inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya maji vijijini ukiwamo ujenzi wa mradi wa kimkakati wa kutoa maji kutoka chanzo cha Chiuwe/Nyangao hadi Ruangwa Mjini wenye thamani ya Sh. bilioni 119 ambao utatoa huduma katika vijiji 34 vya Wilaya ya Ruangwa na vijiji 21 vya Wilaya ya Nachingwea.

Uwekezaji huo utaboresha upatikanaji maji katika vijiji na kufanikisha upatikanaji wa huduma hiyo vijijini kufikia asilimia 72.01 na mjini asilimia 77.

Majaliwa pia alisema serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya michezo ukiwamo ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu wa Majaliwa na hivyo kuongeza hamasa ya vijana kujihusisha na michezo ambayo ni chanzo cha ajira na kuwapatia burudani.

Kwa sasa wilaya hiyo ina timu tatu ambazo ni Namungo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Namungo B na Ruangwa Queens.

**KINANA ALONGA**

Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Kinana, alisema maendeleo makubwa yanayoendelea kufanyika wilayani Ruangwa, yanatokana na kazi nzuri inayofanywa na Mbunge wa Ruangwa na Waziri Mkuu, Majaliwa, ambaye amekuwa kiungo cha karibu anayewaunganisha wananchi, viongozi wa CCM na viongozi wa serikali.

Alisema kasi kubwa ya kupeleka maendeleo inayofanyika Ruangwa ni ya kupigiwa mfano, hivyo akataka wananchi kuendeleza umoja na mshikamano katika kujiletea maendeleo ya kweli.

"Ninampongeza Waziri Mkuu kwa uungwana wake na unyenyekevu wake. Waziri Mkuu ni mtu mtaratibu na muungwana na ndizo sifa ambazo kiongozi anatakiwa awe nazo.

"Mimi nitakuwa shahidi wa kusimulia kazi nzuri ya maendeleo inayofanywa Ruangwa. Mimi ninatembea mara nyingi nchi nzima, nimewahi kupita Ruangwa miaka ya 1980 na 2000, lakini Ruangwa ya leo ni tofauti kabisa na Ruangwa niliyowahi kuiona huko nyuma. Nakupongezeni Wana-Ruangwa kwa umoja na mshikamano wenu," alisisitiza.

Kinana pia alitumia fursa hiyo kuipongeza serikali chini ya uongozi wa Rais Samia kwa kuendelea kufikisha maendeleo katika maeneo mbalimbali na kumfanya avunje rekodi kwa kufikisha fedha nyingi za maendeleo katika halmashauri zote nchini.

"Ndugu zangu sifa mnazompa Rais anastahili kwa kuwa anafanya kazi nzuri ya kuwaletea maendeleo Watanzania," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa CCM pia alisema hakuna dhambi yoyote kwa kiongozi aliyeko madarakani anapomaliza awamu ya kwanza kupewa awamu ya pili aendelee kuongoza.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassan yuko awamu ya kwanza, kwanini asipewe awamu ya pili? Hakuna sababu ya kusema 'hapana!'," Kinana alisema.

Aliongeza kuwa Rais Samia anaonesha njia kwa kupanga, kutafuta mikakati na kuweka vipaumbele na sasa Watanzania wanajivunia mafanikio na hata wana CCM wanaposema mgombea tuliyenaye anatosha kugombea mwaka 2025, ninadhani wana hoja hususan kwa kutambua mchango wake mkubwa katika Taifa hili.

Baadhi ya wananchi wa Ruangwa wakizungumzia utekelezaji ilani katika wilaya yao, walisema wameridhishwa na kasi ya ujenzi wa miradi ya maendeleo na wanaishukuru serikali kwa kutimiza wajibu wake kwa wananchi.

Wananchi hao walisema awali katika wilaya yao kulikuwa na changamoto mbalimbali zikiwamo za upatikanaji huduma bora za afya ambapo kwa sasa imekuwa historia baada ya serikali kuidhimisha fedha kwenda Ruangwa na kufanikisha ujenzi wa hospitali ya wilaya, vituo vya afya na zahanati.

"Kwa sasa hatuna tabu ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya, kila kitu tunakipata hapahapa hadi upasuaji," alisema Tabia Juma, mkazi wa Kata ya Narungombe.

Naye Mzee Abdallah Mtumbe, mkazi wa Kata ya Nandagala, Kijiji cha Nandagala 'A', alisema kutokana na kazi nzuri ya utekelezaji ilani inayofanywa na Rais Samia na serikali yake, hakuna atakayewaambia lolote dhidi ya viongozi wao wakamsikiliza.

"Hatuwezi kuwaacha hawa wote wakati wowote, tumeona utekelezaji wa ilani na maendeleo hapa wilayani, nani anaweza kuyafanya haya yaliyofanyika hapa Ruangwa?" alihoji.

Mwananchi mwingine Mwajuma Makota, mkazi wa Kata ya Nambilanje, Kijiji cha Nanjaru, alisema kwa sasa katika kitongoji chao cha Kiperembende, watoto wanasoma karibu na makazi yao baada ya ujenzi wa shule ya msingi kukamilika na hivyo kuwapunguzia kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 10 kwenda Kijiji cha Nanjaru walikokuwa wanasoma awali.





## ‘Marufuku mabasi ya shule kubeba abiria’

**Na Steven William,** MUHEZA

KIKOSI cha Polisi Usalama Barabarani Wilaya ya Muheza, Tanga, kimepiga marufuku mabasi maalum ya shule kubeba abiria kwenda misibani ama katika harusi kwa kuwa ni kinyume cha sheria.

Mkuu wa kikosi hicho, Leonard Bandola, akizungumza juzi, wakati wa uchunguzi wa magari maalum ya kubeba wanafunzi alisema dereva atakayekamatwa kwenda kinyume na maagizo hayo atachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema kuwa Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani Wilaya ya Muheza kinaendelea na ukaguzi wa magari ya shule ikiwa ni utaratibu wao wa kila mwaka kabla ya muhula wa masomo kuanza.

Bandola alisema kuwa wamekuwa wakifanya ukaguzi wa magari hayo ili kubaini changamoto na kutoa maelekezo ya matengenezo ya vyombo hivyo ambavyo ni mahususi kwa kubeba watoto wa shule mbalimbali katika wilaya hiyo.

Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Muheza, Charles Ntenga, amesema polisi wamekuwa na utaratibu wa ukaguzi wa magari ya wanafunzi kabla ya shule kufunguliwa ili kuweka mazingira salama kwa watoto wanaotumia vyombo hivyo kwenda shule.

Aliwasihi wamiliki na madereva kuitikia wito wa ukaguzi wa vyombo kwa kuwa wataendelea kukagua na kutoa elimu kwa wamiliki wa vyombo hivyo vinavyobeba wanafunzi.

Aidha, alitoa wito kwa wamiliki wa vyombo hivyo kufanya matengenezo na ukaguzi wa vyombo vyao mara kwa mara na wazazi na walezi kufuatilia mwenendo wa magari yanayobeba watoto wao ili kubaini changamoto wanazopitia katika matumizi ya vyombo hivyo.

Kwa upande wake mmiliki wa shule ya Zion English Medium, Mary Meena, alisema Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wilayani Muheza kimefanya ukaguzi huo kwa wakati sahihi.

# RUWASA yapewa siku saba kukamilisha mradi wa maji

**Na Oscar Assenga,** LUSHOTO

NAIBU Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, amemwagiza Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Lushoto, mkoani Tanga, Erwin Sizinga, kukamilisha mradi wa ulazaji wa mabomba kilomita 2.8 ndani ya siku saba.

Pia amemwagiza mkandarasi anayejenga mradi wa maji wa Magamba, kuhakikisha anaongeza kasi ya utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ili aweze kukamilisha kwa wakati.

Alisema lengo la kutoa muda huo ni kuhakikisha wananchi wa Kata ya Ubiri na Ngulwi, wanapata huduma ya majisafi na salama mapema ili kujiepusha na athari ikiwamo magonjwa ya mlipuko.

Mahundi aliyasema hayo jana wakati akizungumza na viongozi mbalimbali, baada ya kukagua utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya maji ya Magamba na mradi wa Maji Irente/Yoghoi/Ngulwi iliyoko Lushoto.

Alisema mradi huo ukikamilika kwa wakati utawaokoa na adha ya shida ya maji wananchi 30,835 kwenye maeneo ya Magamba, Kwesimu, Bara, Jegestal, kambi namba nne, Chakechake, Kitivo, Maguzoni, Sinza, Lushoto Mjini, Mabwawani, Kipembe na Kialilo .

"Meneja wa RUWASA wa Wilaya hii lazima uhakikishe wananchi katika maeneo hayo wapatao 30,835 wanapata huduma ya maji ili kuwaondolea adha wanayokumbana nayo," alisema Naibu Waziri Mahundi.

Mbunge wa Lushoto, Shaban Shekilindi, aliishukuru serikali kwa kutekeleza miradi ya maji kwenye jimbo hilo huku akisema wananchi wengi watapata huduma ya maji.

Mbunge Shekilindi, pia alisisitiza makandarasi wanaotekeleza miradi hiyo kuikamilisha kwa wakati ili wananchi wapate huduma hiyo muhimu.



Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Mohamed Mfaki (kushoto), akikagua uandikishaji wa wanafunzi wanaoingia darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Kwemkabala wilayani Muheza jana. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# DC ashauri bandari bubu kuwa rasmi

**Na Oscar Assenga,** PANGANI

MKUU wa Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga, Zainabu Abdallah, ameishauri Wizara ya Uchukuzi, kuipandisha hadhi bandari bubu Mkwaja iliyoko wilayani humo, kuwa bandari rasmi kwa ajili ya kusafirisha mifugo.

Zainabu, aliwasilisha ombi hilo jana kwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, aliyefanya ziara wilayani humo kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa.

Alisema amelazimika kuwasilisha ombi hilo kutokana na Bandari ya Mkwaja, kuongoza kwa kusafirisha mifugo. Kwa mwezi mmoja, bandari hiyo hupitisha ng'ombe zaidi ya 2,500 na kwa mwaka ni zaidi ya ng'ombe 30,000.

Aidha, Mkuu huyo wa Wilaya, alisema usafirishaji huo unafanyika huku kukiwa na miundombinu duni hivyo kuomba ipandishwe hadhi na kuwa bandari rasmi ili itumike kwa kazi maalum ya kusafirisha mifugo.

"Tunatambua bandari zipo nyingi lakini kwa sababu Bandari ya Mkwaja ipo ukanda wa Kaskazini ambapo shughuli nyingi za mifugo zinafanyika kama ilivyokuwa Kilwa kupewa hadi ya kuwa na bandari ya uvuvi hivyo ikikupendeza mamlaka Bandari ya Mkwaja iwe maalumu kwa ajili ya mifugo," alisema.

Alisema wawekezaji wenye boti za kisasa wapo tayari kuchukua mifugo na kupeleka nchi za Falme za Kiarabu lakini wanarudishwa nyuma na changamoto ya miundombinu.

"Lakini wananchi wa Mkwaja wataneemeka, uchumi wa Mkwaja utafunguka na uchumi wa wilaya na maendeleo yatakua kwa kasi kubwa," alisema.


Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Wilaya, serikali imeboresha miundombinu ya Bandari ya Pangani ikiwemo kuweka boya lililogharimu zaidi ya Sh.milioni 400.

Lengo la maboresho hayo ni kurahisisha boti za abiri na mizigo kutia nanga katika gati ya Pangani hatua ambayo inatoa fursa kwa wafanyabiashara na wamiliki wa boti za abiria na mizigo sasa kufungua safari za Pangani.

Licha ya maboresho hayo, serikali imetoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa soko la kimataifa la uvuvi ambalo litaifungua Bandari ya Kipimbwi.

Akiwa Pangani, Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alisema k wamba ziara hiyo ni ya kukagua Bandari ya Pangani, Kipumbwi na Mkwaja; na hayo ni matunda ya Pangani Investment Forum inayolenga kufungua milango kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza wilayani humo.

"Kwa kweli kuja kwangu mimi ni moja ya matunda mazuri ya forum ya uwekezaji ya kuwekeza Pangani iliyoandaliwa na Mbunge, DC na Halmashauri na malengo yenu yalikuwa ni kufungua bandari hii kuwa ya mifugo na Bandari ya Kipumbwi kuwa ya Uvuvi," alisema Naibu Waziri huyo.





# Waandamana kutaka sekondari ijengwe kwenye eneo lao

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Kijiji cha Nyabusalu, Kata ya Bulungwa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wameandamana hadi katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama kupinga sekondari mpya kujengwa Kijiji cha Makongolo na badala yake wanataka ijengwa kwenye kijiji chao.

Sababu za kuchukua uamuzi huo inaelezwa ni kutaka kuwanusuru wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya elimu kama shule hiyo itajengwa katika Kijiji hicho.

Kata hiyo yenye vijiji tisa inaelezwa kuwa na shule moja tu katika Kijiji cha Mseki na kusababisha wanafunzi wanaotoka vijiji vya pembezoni kutembea umbali wa kilometa nane hadi 15 kusaka huduma hiyo.

Mwenyekiti wa serikali ya Kijiji cha Nyabusalu Robert Maganga akiongoza maandamano hayo alisema, makubaliano ya awali ya kujengwa kwa Sekondari mpya katika kijiji hicho yalielezwa na diwani wa Kata katika mkutano wa hadhara na baadae kujadiliwa kwenye kikao cha kamati ya maendeleo ya Kata (WDC).

Kufuatia uamuzi huo, Desemba 10 mwaka jana walikubaliana kutenga eneo la ujenzi wa sekondari hiyo lenye ukubwa wa hekari 65 na kuandaa mawe ya kuanzisha ujenzi huo.

Alisema Desemba 12 waliandika muhtasari wa makubaliano na kuuwasilisha kwa Mkurungezi wa Ushetu ili kuja kukagua eneo hilo kwa ajili ya kuanza kwa ujenzi wa shule hiyo.

Maganga alisema, Mkurugenzi aliwapongeza kwa hatua ya kutenga eneo hilo na siku kadhaa baadae alituma watalaamu wake kukagua eneo, badala yake walielekezwa na diwani kwenda eneo jingine lililopo Kijiji cha Makongolo ambapo ni jirani na sekondari iliyopo.

Mwenyekiti wa Kamati ya shule ya Msingi Nyabusalu Mihayo Kanamanza alisema, wameandamana ili kushinikiza sekondari hiyo kujengwa kijijini hapo na kuwaondolea adha ya wanafunzi kutembea umbali mrefu. Mmoja wa Wazazi walioandamana,Matha Bahati alisema, hawana nia mbaya kuandamana kwani lengo ni kushinikiza kujengwa kwa sekondari katika eneo ambalo awali walikubaliana ili kusaidia wanafunzi. Ofisa Tarafa wa Isagehe, Vincent Ndesekio, aliyewapokea baada ya kufika ofisi ya Mkuu wa Wilaya, aliwasikiliza kilio chao na kuahidi kulifikisha kwa Mkuu wa Wilaya, Mboni Mhita ili atapore-jea kutoka safari na kufika kwenye eneo hilo kuzungumza nao na kupata ufumbuzi.




Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, akigawa daftari na kalamu kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao wameanza masomo jana katika Shule ya Sekondari Ngokolo Manispaa ya Shinyanga, akiwa ziarani kukagua maendeleo ya wanafunzi walioripoti shuleni muhula huu wa masomo 2024. **PICHA: SHABAN NJIA**

# SHUWASA yakusanya mil.29/- kutoka kwa wahujumu maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), imekusanya faini ya Sh.milioni 29.16 kutoka kwa watu 76 waliowakamata wakiwaibia maji.

Mkurugenzi Mtendaji wa SHUWASA, Mhandisi Yusuph Katopola, alibainisha hayo juzi wakati akitoa taarifa ya miaka mitatu ya utekelezaji katika taasisi hiyo kwa waandishi wa habari.

Alisema wamefanya kazi ya kuboresha utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi, lakini wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la baadhi ya watu ambao siyo waaminifu kuwaibia maji, na wamekuwa wakiwatoza faini ambazo mpaka wameshaingiza Sh.milioni 29.16 kuanzia mwaka 2021 hadi 2023.

Aidha, alisema ndani ya miaka hiyo, wametekeleza miradi 10 ya maji yenye thamani ya Sh.bilioni 8.5,kati yao saba imekamilika na mitatu bado inaendelea kutekelezwa na itanufaisha wananchi 116,249.

Alisema pia serikali kupitia Wizara ya fedha, ilisaini Mkataba wa fedha na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) Euro Sh.milioni 76 mkopo wa riba nafuu sawa na Sh.bilioni 200, fedha ambazo zitatumika kuboresha zaidi utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi na kufikiwa maeneo yote.

Alisema mbali na fedha hizo kutoka kwa wafadhili, wanatarajia kukopa benki Sh.milioni 735.4 ambazo zinatumika kukarabati ujenzi wa mradi wa kuchakata majitaka, ili kufikia mita za ujazo 100 kutoka mita za ujazo 40, na kununua gari lao la majitaka.

Vilevile alisema Mamlaka hiyo imepanua mtandao wa utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi, ambapo awali ilikuwa ikiwahudumia wananchi wa Manispaa ya Shinyanga pekee, lakini sasa ina hudumia na Miji ya Tinde, Didia na Iselamagazi wilayani Shinyanga.

"Upatikanaji wa huduma ya maji mpaka sasa kwa Shinyanga Mjini ni asilimia 92, na pembezoni mwa mji ni asilimia 58, na miradi hii ambayo tunakwenda kuitekeleza ikikamilika huduma ya maji maeneo ya mjini itakuwa asilimia 100 na pembezoni asilimia 95," alisema Katopola.

Katika hatua nyingine alisema Mamlaka hiyo imefanikiwa kupunguza tatizo la upotevu wa maji, kutoka asilimia 26 mwaka 2020/2021 hadi asilimia 11mwaka jana, na mwaka 2022 walipata tuzo ya kudhibiti upotevu wa maji kati ya mamlaka za maji 26 za Mikoa, kwa kudhibiti kwa asilimia 16.

Alitoa wito pia kwa wananchi wa Shinyanga kuendelea kuchukua tahadhari ya kudhibiti upotevu wa maji, na kuacha kuwaachia watoto wakichezea mabomba, ili kuepuka ongezeko za bili za maji kuwa kubwa na kuanza kulalamika.

# Bil.41/- zamwagwa Manispaa Tabora

**Na Halima Ikunji,** TABORA

SERIKALI imeipatia Manispaa ya Tabora Sh.bilion 41.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo kuboreshwa miundombinu ya elimu na afya katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024.

Hayo yalibainishwa juzi na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Seif Salum, alipokuwa akiongea na waandishi wa habari ofisini kwake na kutaja fedha hiyo kuwa chachu katika upatikanaji huduma za jamii.

Alitaja sekta ambazo zimefanyiwa maboresho makubwa ya utoaji huduma kuwa ni elimu, afya, barabara, maji, kilimo na utawala ambapo zimejengwa nyumba bora za watumishi na kutoa usafiri kwa watendaji ili kuwarahisishia kazi.

Alisema Halmashauri hiyo ilipokea Sh.bilioni 6.4 kwaajili ya uboreshaji miundombinu ya afya katika hospitali ya wilaya ikiwemo kununua vifaa tiba vya kisasa.

Alitaja baadhi ya huduma zilizoboreshwa katika Hospitali hiyo kuwa ni pamoja na kujengwa wodi ya kisasa ya kujifungulia akinamama wajawazito pamoja na jengo la kisasa la kutolea huduma ya mionzi.

Vilevile alitaja baadhi ya vituo vya Afya na Zahanati vilivyopo katika Kata na Vijiji mbalimbali kuwa vimefanyiwa maboresho makubwa na nyingine zikiwa katika hatua mbalimbali za ujenzi ili kuwezesha wananchi kupata huduma bora za Afya.

Kuhusu miradi ya elimu msingi alisema wamepokea Sh.bilioni 8.2, kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya, vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na nyumba za walimu pamoja.

Aidha alisema wamepokea Sh.bilioni 17.7 kwa ajili ya uboreshaji miundombinu ya shule kongwe za sekondari ya Tabora wavulana, Tabora wasichana, Milambo na Kazima pamoja na ujenzi wa shule mpya katika baadhi ya Kata. kutenga eneo la ujenzi wa sekondari hiyo

Nipashe
TESA
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI
Jumanne Januari 9, 2024



Ukurasa 13

## BAADA YA RUHUSA UTAFITI GMO...
# Wataalamu waitaja kanuni kuwajibika, kufidia inavyowabinya uwekezaji wa bayoteknolojia



Ukurasa 14

Vijana wanavyovutiwa na kuhusudu bangi, picha yake pambo la magari, boda na mwili

NA MICHAEL ENEZA

# Ni wiki ya walimu, wanafunzi kuanza majaribio mapya mfumo wa elimu

SHULE zinapofunguliwa wiki hii, walimu na wanafunzi watajikuta katika mambo mapya, kubadili mapana na marefu ya majukumu yao.

Ni kwa walimu hasa mpangilio wa masomo wanaoufahamu tangu waanze kazi, au wakiwa masomoni.

Licha ya kuwa maamuzi muhimu tayari yalishafanyika kutakuwa na wakati wa kujifunza na kupima, kwanza kwa suala la ufanisi wa kufundisha, kusoma na kufaulu au kufaulisha, halafu kubwa zaidi, uhusiano wa hali hiyo na kuingia soko la ajira.

Inaweza kuchukua muda ili kupata majibu; labda hawangoji majibu bali yapo maslahi ya badiliko hilo.

Pengine mpangilio wa mabadiliko hayo haujaeleweka kikamilifu kwani viashiria kwa kiasi fulani vinatofautiana, kwanza maelezo kuwa mfumo mpya wa elimu ya msingi pamoja na sekondari unaanza kutumia mwaka 2026 shule zikianza muhula mpya wa masomo.

Halafu yapo maelezo kuwa mpangilio wa ufundishaji, masomo yatakayotolewa, mabadiliko hayo yanaanza kufanyiwa kazi sasa, yaani kuingizwa rasmi darasani, kuanzia mwaka mpya wa masomo 2024.

Kuna wasiwasi kuwa viwango vya kujipanga bado ni kitendawili, kwa mfano ni shule ngapi zitakuwa na waalimu wa kufundisha Kiingereza kama somo kuanzia darasa la kwanza kama mpango huo unaanza kutekelezwa sasa bila maandalizi makubwa ya walimu.



Wanafunzi katika mkusanyiko wa kishule. PICHA: UNICEF

Mpangilio mpya wa ufundishaji shuleni unatakiwa kukidhi mahitaji shindani ya kijamii, hasa lile la kujimudu kuunda au kutafuta vyanzo vya kipato bila kutegemea ajira katika mfumo rasmi.

Tatizo la mwelekeo huo unapoingizwa katika mtiririko wa kinachofundishwa ni kuwa hitaji hilo ni ongezeko la mitaala ambayo inabidi iwepo shuleni, na kwa upande mwingine, ni kuwepo kwa taasisi maalum za kuwaandaa wahitimu kwa mielekeo ya kiufundi ili kubuni njia za kujitegemea.

Ni hapo kuna msuguano wa kubadili mitaala wakati kinachotakiwa ni taasisi tofauti za nyongeza, na hivi sasa kila wilaya inajenga chuo cha ufundi wa nyanja mbalimbali.

Ina maana kuwa kwa mtazamo wa kawaida, hakuna haja ya kubadili mambo katika mitaala ila kuunda taasisi hasa katika ngazi ya wilaya kutoa mafunzo kwa wahitimu kupata njia za kipato, kulingana na walikofikia kimasomo.

Huenda kuingiza suala la ajira katika masomo ni kubadili darasa liwe la ufundi badala ya ufahamu, hali ambayo inaumiza uwezo wa uelewa katika masomo yanayofuatia ngazi hiyo ya ufundishaji ambayo itakuwa imeingiliwa kitaaluma.

Wanaohitimu katika ngazi hiyo watakuwa hawajapata masomo yanayohitajika kukamilisha hatua hiyo, kama sehemu isiyo ndogo ya muda wa masomo itakuwa imechukuliwa na kuingiza ufundi, wakati kuna vyuo vyake.

Kwa upande mmoja hitilafu zinazoweza kujitokeza zinaanzia katika dhana potofu kuwa masomo yanalenga kufaulu mitihani na siyo kujiajiri, na hata kwa jinsi dhana hiyo inavyotamkwa, ni wazi anayezungumza huenda haoni lolote la maana katika huko 'kufaulu mitihani, anaweka mkazo katika 'kujiajiri.'

Inaweza kuwa hiyo pia ni dhana potofu yenye maana kinzani kadhaa,mosi ikiwa ni kutafuta kuwa kibarua hapa au pale katika nyakati tofauti kwa mfano katika ujenzi wa nyumba, kwani tayari mwanafunzi anaujua ujenzi.

Akiweza kupata mkopo au msaada akanunua vifaa anaweza kuwa fundi wa kujitegemea, aangalie ni wapi kuna uhaba wa mafundi iwe ni mtaa, wilaya au kijiji akae huko.

Dhana ya kujiajiri ina tatizo la kimantiki, kwamba kijana anakuwa mtafuta kazi na mtoa kazi, mhitaji ajira na mtoa ajira jambo ambalo haliwezekani. Utunzi wa dhana hiyo ni kulazimisha kuridhika na kubangaiza, useme ni ajira, kwa kukwepa ukweli kuwa kijana huyo ameanzisha biashara, kwa mfano uchuuzi wa kupeleka nguo huku na kule. Unaposema 'amejiari' kunakuwa na dhana ya kuridhika na hali aliyo nayo kama ajira, kuwafundisha wengine wasitegemee 'ajira za serikali.

INAENDELEA UK. 12

ELIMU

## NA SABATO KASIKA

# Mara inapoanza masomo na uhaba walimu wa 'mathe' na sayansi

■ Ni shule za umma, wastaafu na wanaojitolea wanapokuwa kimbilio



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, akizungumza katika mkutano wa kutathmini maendeleo ya elimu mkoani humo. PICHA: MPIGAPICHA WETU

UHABA wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati ni kama ugonjwa unaoelekea kuwa sugu kwenye sekondari kuanzia za kata vijijini na hadi kongwe mijini na kwenye majiji .

Ni changamoto inayozikumba sekondari za umma na kusababisha wanafunzi kuboronga kwa vile hawafundishi kikamilifu masomo hayo.

Hata ufundishaji Kiingereza pia unasuasua na kusababisha Baraza la Mitihani ya Taifa (NECTA) mwaka jana kueleza kuwa wanafunzi wanafeli kwenye somo hilo ambalo linashika ufunguo wa mawasiliano kimataifa.

Kwa upande wa sayansi na hisabati Mara ni miongoni mwa mikoa yenye uhaba wa walimu wa masomo hayo na kusababisha watumike walimu wanaosubiri ajira na waliostaafu kwa kulipwa posho.

Hayo ni kwa mujibu wa Kaimu Katibu Tawala Msaidizi (elimu wa mkoa), Makwasa Bulenga, anayaeleza hayo kwenye kikao cha tathmini ya maendeleo ya elimu mkoa wa Mara.

Katika ufafanuzi wake, Bulenga anasema mkoa huo una shule za sekondari za umma 263 na walimu wa masomo ya sayansi na hisabati waliopo ni 1,021 wakati mkoa unahitaji 1,910, na kwamba kuna upungufu wa walimu 889 katika shule mbalimbali za sekondari za umma.

"Uhaba huo unasababisha shule zitumie walimu wa masomo hayo wanaosubiri ajira na wastaafu ambao wanalipwa posho za kujikimu kutegemea jinsi wazazi na bodi za shule wanavyokubaliana," anasema Bulenga.

Anaongeza kuwa njia nyingine wanayotumia ni kuomba walimu kutoka shule zenye walimu wa masomo hayo kuwa na vipindi katika shule za jirani zisizo na walimu wa masomo hayo.

"Uhaba huu wa walimu unaathiri ufundishaji wa masomo hayo katika shule mbalimbali za sekondari mkoani kwetu," anasema Bulenga mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Mara Said Mtanda.

Aidha, anaeleza kuwa wakati shule zikikabiliwa na uhaba wa walimu wa masomo hayo, lipo pia tatizo la baadhi ya wazazi kutochangia chakula shuleni.

"Kwa shule za msingi ni asilimia 42 ya wanafunzi wanaokula chakula shuleni, kwa sekondari ni asilimia 49, hivyo tuna changamoto hiyo," anasema Kaimu Katibu Tawala Msaidizi upande wa elimu wa mkoa.

Anasema, suala la chakula shuleni halikwepeki, na kwamba ni muhimu wazazi na walezi walielewe hilo, kwa kuwa mwanafunzi anapokuwa amekula anakuwa na usikivu, uelewa na juhudi kwenye masomo.

"Kutokula chakula shuleni kunachangia utoro, kujiiingiza kwenye uhalifu hivyo wazazi na walezi waachane na kauli kwamba serikali inatoa elimu bure."

Anawahimiza kuwajibika kugharamia chakula cha watoto wao, kuwahamasisha kusoma na kuwajengea msingi bora wa kupenda elimu.

**ONGEZENI UBUNIFU**

Ni rai ya Mkuu wa Mkoa Said Mtanda, anawataka walimu na wasimamizi wa elimu katika ngazi mbalimbali kuongeza ubunifu na kujiongeza katika utendaji kazi ili kuchochea mabadiliko chanya kwa walimu na wanafunzi.

"Sio lazima mtu uwe na cheo kikubwa ndiyo ufanye mabadiliko, unaweza kuwa huna cheo lakini kwa namna unavyochapa kazi na kuongeza ubunifu unaweza kuleta mabadiliko makubwa katika eneo lako kuliko hata mtu mwenye madaraka makubwa ambaye hana ubunifu," anasema Mtanda.

Aidha, anawataka walimu kujiendeleza kimasomo na kuchangamkia fursa mbalimbali zilizopo katika maeneo yao ya kazi.

"Lakini wakurugenzi wa halmashauri ambao hawajakamilisha ujenzi wa shule mpya na kuzisajili, fanyeni kazi usiku na mchana na kuhakikisha mnasajili shule hizo mapema, ili ziweze kuanza kuchukua wanafunzi Januari, 2024," anasema.

Aidha, Mkuu wa Mkoa anawataka wakurugenzi na wasimamizi wa elimu katika ngazi mbalimbali kuwasikiliza walimu na kujitahidi kutatua baadhi ya changamoto zao zinazowakabili ambazo zipo katika ngazi yao na hauhitaji fedha.

"Wekeni malengo katika utekelezaji wa majukumu yenu na katika maisha yao binafsi na kuisemea vizuri serikali kwa mambo mazuri inayoyafanya kwa wananchi wa Mkoa wa Mara," anasema.

**KUUA DIRA**

Mhadhiri wa Chuo Cha Diplomasia Kurasini Dar es Salaam, Abbas Mwalimu , akizungumzia uhaba wa walimu wa sayansi na hisabati, anasema shule za umma kukosa walimu hao ni sawa na kuua dira ya maendeleo.

Anasema, ili kuwa na kizazi chenye ubunifu, wataalamu na wajuzi wa masuala ya sayansi na teknolojia ni lazima kukitengezea mazingira ya kufanikisha ubunifu huo pamoja na uvumbuzi hasa wakati wa karne hii ya ubunifu na ugunduzi.

"Dira ya maendeleo inahitaji kizazi chenye ubunifu na uvumbuzi hasa kwenye mabadiliko ya nne ya viwanda, hivyo ni muhimu kuwekeza kwenye sayansi kwa kuwa na walimu wa kutosha wa masomo ya sayansi kote nchini," anasema Mwalimu.

Anasema, wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi ndio wanaotarajiwa kuwa wabunifu wa baadaye, wataalam wa fani mbalimbali kuanzia wahandisi, madaktari na wengine wengi, lakini wanaweza wasifikie huko kutokana na uhaba wa walimu.

"Njia nzuri ni serikali kuona tatizo na kulifanyia kazi haraka ili nchi iweze kuwa na wabunifu, wavumbuzi na wataalamu wengi wa baadaye. Kimsingi tunahitaji kuwa na jamii ambayo ina ubunifu," anasema.

Mwalimu anasema, kama nchi inataka kuwa na wataalam wa kutosha wa baadaye na sasa uwekezaji wa kutosha kwa walimu wa masomo ya sayansi haukwepeki.

# Ni wiki ya walimu, wanafunzi kuanza majaribio mapya mfumo wa elimu

**INATOKA UK. 11**

Ingefumuliwa kwa mageuzi ya haja sekta zote zinazohusika zingetoa ajira nyingi , kampuni nyingi zikitoa huduma bora.

Ina maana kuwa mfumo wa elimu unayumbishwa kwa sababu serikali inajaribu kutoa elimu sambamba na vyuo vya ufundi ambayvo sasa vinajengwa kila wilaya.

Ingefaa mitaala ya ufundi iwekwe pembani ibaki ile ya uelewa halisi na iboreshwe na hapo ndipo kufundisha Kiingereza kuanzia darasa la kwanza ungeingia.

Suala hilo siyo dogo kwani msingi imara zaidi wa Kiingereza iwapo angalau watapatikana waalimu, unampa mwanafunzi uwezo zaidi wa kusoma na kuelewa, ingawa bado kuna mtihani kama baada ya darasa la sita Kiingereza kitakuwa bado ni lugha ya kufundishwa kama somo au kitakuwa ni lugha ya kufundishia kama mfumo ulivyo sasa.

Suala hili siyo dogo kwani kuondoa mtihani wa darasa la saba na kuingia moja kwa moja sekondari halikuanza kutokana na hitaji la kuboresha mitaala ila kuendeleza ufundishaji kwa Kiswahili kwa kutokuwepo na badiliko rasmi kutoka ngazi moja hadi nyingine kwa mchujo halisi.

Kutoka mwaka 2014 hadi sasa mazingira ya kuingizwa mkakati huo katika mitaala yamebadilika, na siyo tena kubadili lugha ya kufundishia kwa kuondoa mitihani na kuendelea darasani chumba kingine ila upanuzi wa elimu ya sekondari kuwa takriban ya wote. Ilipokuwa bado finyu na hasa pale ikiwa na malipo maalum, kuondoa mtihani darasa la saba isingewezekana.

Hivi sasa kuna lengo pengine kubwa zaidi kuliko hili la matumizi ya lugha ya taifa kuwa ndiyo itumike sekondari, kwani hata moto wa kupigania jambo hilo inaelekea kuwa umepungua.

Mwelekeo wa sasa unahitaji kuondolewa darasa la saba ila kuwepo na mtihani wa majaribio, ambao sasa umewekwa darasa la sita ili mwanafunzi ajisikie bado yungali shuleni na siyo kamaliza ngazi fulani muhimu ya masomo, ili kupambana na vikwazo vinavyisababisha utoro na kukwama kusoma.

Wako wanafunzi wengi wanaofanya vibaya hata kwa makusudi ili waondoke shuleni wapo waolazamoshwa kuolewa au wengine wanataka kuhamia katika uvuvi au kuchimba madini.

Kuhakikisha kuwa elimu ya sekondari inafuata papo kwa papo kwa kupunguza kidogo muda wa elimu ya msingi ili ikatishwe na ya sekondari ianze bila kutoa mwanya wa kuwa na wanafunzi wengi waliopevuka wanaoangaliwa kwa jicho lingine mitaani au vijijini, ni njia halisi ya kuhakikisha kuwa hakuna masuala kama ndoa kabla ya umri wa miaka 18.

Siyo rahisi kwa mwanafunzi kumaliza sekondari kabla ya umri huo, na kwa jumla itajenga msingi bora zaidi wa uelewa endapo viwango vya kufundishia vitaboreshwa, na siyo kuendeleza elimu ya msingi kwa njia nyingine.

Unaweza kusema bado kuna tatizo la kisaikolojia kama kutokufanya mtihani na kufaulu kuingia rasmi sekondari kunaweza kuwa na athari miongoni mwa wanafunzi au walimu, wanavyoangalia masomo au wanavyojiandaa.

TEKNOLOJIA

NA BEATRICE PHILEMON

## BAADA YA RUHUSA UTAFITI GMO...

# Wataalamu waitaja kanuni kuwajibika, kufidia inavyowabinya uwekezaji wa bayoteknolojia

UNAPOZUNGUMZIA bayoteknolojia ya kisasa inawezekana si Watanzania wengi wanaoifahamu. Utalaamu huo, unaofahamika pia kama uhandisi jeni au mabadiliko ya kijenetiki, ni ujuzi unaohusisha kuhamisha jeni au kinasaba kinachobeba sifa inayohitajika kutoka kiumbe kimoja kwenda kingine na kupata kingine kilichoboreshwa kijenetiki.

Kiumbe kilichoboreshwa kijenetiki au 'Genetically Modified Organism- GMO', huhusisha wanyama na mimea ambao hubeba sifa au tabia bora zinazohitajika, mojawapo ikiwa ni ukinzani na maradhi na uwezo wa kuhimilia mazingira magumu hasa mimea.



Mlezi wa Chama cha Bayoteknolojia Tanzania, Adam Malima

Iwapo taifa litatumia fursa zinazotokana na matumizi sahihi na endelevu ya bioteknolojia linaweza kubadili sekta kuu za uzalishaji hususan kilimo na viwanda na kuzifanya za kisasa na zenye tija zaidi, anasema Adam Malima.

Pia wakulima pamoja na wadau mbalimbali katika mnyonyoro wa thamani watapata wigo mpana na nyenzo bora za kukabiliana na changamoto za uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara na hivyo kukidhi mahitaji ya chakula, uzalishaji wa malighafi za viwandani na kuuza nje ili kupata fedha za kigeni.

Malima mlezi wa Chama cha Bayoteknolojia Tanzania (BST),anawaambia wadau katika mkutano mkuu wa mwaka 2023 unaofanyika Dar es Salaam hivi karibuni.

Ukiwa na kauli mbiu 'Ubunifu wa Bayoteknolojia na Suluhu katika Kujenga kesho iliyo Bora'

Anahimiza serikali kuimarisha utafiti wa bayotekolojia kwenye sekta ya kilimo ili kupata suluhisho la baadhi ya changamoto zinazowakabili Watanzania.

Hatua hiyo pia itatoa fursa na hamasa kwa wahitimu wa vyuo ndani na nje kutumia utaalamu wao kunufaisha taifa.

Anasema serikali iendelee kuwajenga uwezo wataalamu, miundombinu na vitendea kazi ili kuendeleza na kusimamia utafiti na matumizi salama na endelevu ya bioteknolojia katika sekta mbalimbali bila kuleta athari hasi kwa binadamu, wanyama na mazingira.

Mbali na hilo, serikali iendelee kuweka mazingira wezeshi ya kisera, sheria na kiutawala yatakayowavutia na kuhamasisha wadau wa ndani na nje kushirikiana na taasisi na wataalamu wa Tanzania kujenga uwezo katika nyanja hiyo.

**UELEWA BAYOTEKINOLOJIA**

Malima anaeleza kuwa uelewa wa masuala ya bayoteknolojia miongoni mwa wanasiasa, watendaji wa serikali, wataalam na jamii ni mdogo, na kukutaka chama BST kuelimisha wananchi kuhusu sera, sheria, mifumo, kanuni na miongozo ya uendelezaji wa bioteknolojia.

Anasema hiyo itaondoa au kupunguza hofu inayotokana na dhana potofu kuhusu teknolojia hiyo.

"Ni vizuri kutoa elimu kwa sababu uelewa na ufahamu wa baadhi ya wadau kuhusu matumizi ya bidhaa zake ni mdogo na hili limesababisha ongezeko la taarifa zisizo sahihi kuhusu teknolojia hii na zenye kuleta hofu kwa jamii," anasema.

Athari kwa afya ya binadamu na wanyama, aidha, bidhaa zinazotokana na mazao ya bayoteknolojia zinachangia kuharibu mazingira, kuwafanya watumiaji kuwa tegemezi na watumwa wa kampuni kubwa ya nje ni miongoni mwa baadhi ya hoja zinazotokana na dhana potofu, anasema Malima.

Matukio kama haya hutokea kila bidhaa mpya zinapoletwa sokoni kwa kutiliwa shaka na baadhi ya watu, kama ilivyojitokeza katika kukubalika kwa matumizi ya chanjo ya UVIKO-19, anasema Mlezi wa BST.

Anawaambia wajumbe kuwa hoja hizo hazina ukweli kwa sababu mchakato wa kutathmini madhara hufanywa kwa kina na wataalamu kabla ya bidhaa kuidhinishwa kwa matumizi.

Taarifa kutoka CODEX Alimentarius, European Food Safety Authority (EFSA) na Shirika la Afya Duniani (WHO), zinasema bidhaa zinazotokana na bayoteknolojia ambazo hadi sasa zimeidhinishwa kuingia sokoni hazijasababisha madhara. yaliyothibitishwa kitaalamu kutokea kwa binadamu, wanyama wala mazingira.

Malima anashauri sekta binafsi ishirikiane na serikali kuendeleza matumizi ya aina zote za bayoteknolojia ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa miche bora ya mazao kama muhogo, migomba, mananasi, viazi vitamu, mviringo na kahawa kwa njia ya tishu au 'tissue culture'.

"Nikiwa mdau wa bayoteknolojia, natambua nafasi na umuhimu wa sayansi, teknolojia na ubunifu katika kuleta maendeleo endelevu nchini, kwani jamii ambayo ina matumizi kidogo ya sayansi na teknolojia itakuwa nyuma kimaendeleo kiuchumi na kijamii," anasema Malima.

Anakumbusha kuwa katika sekta ya afya matumizi ya bayoteknolojia yamerahisisha na kuongeza ufanisi kwenye utambuzi wa magonjwa kwa usahihi.

Aidha, anasema imewezesha kutengeneza chanjo za UVIKO-19, homa ya ini (hepatitis B), saratani ya shingo ya kizazi, malaria, pia imefanikisha kuzalisha dawa mpya na zenye ubora zaidi kukabiliana na magonjwa sugu kwa mfano insulin kwa ugonjwa wa kisukari, VVU na UKIMWI, kuharisha kwa watoto (rotavirus) na malaria.

Katika sekta ya kilimo, Malima anasema matumizi yake yamezalisha miche bora isiyo na vimelea vya magonjwa, ugunduzi wa aina bora za mbegu mbalimbali zinazozaa sana, zenye ukinzani dhidi ya magonjwa na wadudu, kupunguza matumizi ya viuatilifu ambavyo vina madhara makubwa kwa mazingira, pamoja na kupunguza gharama za uzalishaji.

"Kwenye mifugo na uvuvi imerahisisha utambuzi wa magonjwa kwa usahihi, kuongeza uzalishaji wa aina bora za mifugo na samaki, pamoja na kutengeneza dawa na chanjo mbalimbali," anaongeza.

Wakati katika sekta ya viwanda, matumizi ya bayoteknolojia yameongeza ufanisi na tija kutengeneza bidhaa mbalimbali za vyakula, pamoja na dawa na kemikali kwa matumizi ya kilimo, afya, mifugo na viwanda.

Mwenyekiti wa Chama cha Bayoteknolojia Tanzania (BST), Profesa Peter Msolla, anasema matumizi yake duniani yameleta manufaa makubwa kwenye sekta za kilimo, afya, mifugo, viwanda na mazingira.

"Hapa nchini, yameleta mafanikio makubwa katika sekta ya afya, hata hivyo kwenye kilimo maendeleo siyo ya kuridhisha sana kwa sababu ilifika wakati hata serikali, kupitia Wizara ya Kilimo, ilipiga marufuku matumizi ya teknolojia hii katika utafiti wa kilimo kwenye taasisi zake," anasema Profesa Msola.

Anasema BST inaishukuru serikali kwa uamuzi wa hivi karibuni wa kuruhusu teknolojia hiyo itumike katika utafiti.

Katika kuhakikisha kuwa taifa linanufaika na utafiti na matumizi sahihi na endelevu ya bayoteknolojia, serikali imeandaa na kupitisha Sera ya Taifa ya Mazingira (2021) na maboresho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira 2004, anasema Mwenyekiti wa BST.

Anaongeza kuwa sambamba na maboresho ya sheria, kanuni mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kanuni za matumizi salama ya bioteknolojia ya (2009) na marekebisho yake ya 2015 yatapitiwa ili zishabihiane na maelekezo ya sera na mabadiliko ya sheria.

"Tunapenda kuipongeza serikali kwa kuchukua hatua za kushirikisha wadau katika zoezi hili na sisi kama chama tumejipanga kushiriki kikamilifu." Anasema.

**CHANGAMOTO**

Akizungumzia mambo yanayokwamisha maendeleo ya bayoteknolojia, anasema ni uelewa na ufahamu mdogo kwa baadhi ya wadau kuhusu matumizi na bidhaa zitokanazo na teknolojia hiyo.

Pia kanuni za kusimamia matumizi salama zimeweka mfumo wa uwajibikaji na kulipa fidia au 'strict liability', unaopelekea kupoteza au kupunguza ushirikiano kati ya taasisi za ndani za utafiti na wadau wa maendeleo katika kuendeleza teknolojia hiyo.

Pia uwezo mdogo wa kutafiti na kuzalisha bidhaa zitokanazo na bayoteknolojia ya kisasa kwa kukosa miundombinu ya kisasa, maabara, vifaa na watu wa kutosha, anaongeza.

Kuwepo na ongezeko la taarifa zisizo sahihi na za upotoshaji zinazosambazwa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhusu teknolojia hiyo pia ni changamoto anayoitaja.

"Taarifa hizi zinaleta hofu na wasiwasi kwa jamii na zinapunguza kasi ya utafiti na kuendeleza teknolojia hii nchini." Anasema Mwenyekiti wa BST.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Vijana wanavyovutiwa na kuhusudu bangi, picha yake pambo la magari, boda na mwili

## • Mtaalamu ahusisha na kusaka faraja

UKIANGALIA namna vijana wanavyoutukuza mmea wa bangi kwa kujipamba na mavazi yenye picha zake na pia kuzibandika kwenye maeneo mbalimbali, utajua wana mahaba na marijuana.

Unaweza kuwaza hivyo kwa sababu wengi wanaonekana kama wanafurahia mmea huo tena wakiuita jani, na kwa jinsi wanavyoupa nafasi kwenye mambo yao.

Katika maeneo mbalimbali mijini kuanzia Dar es Salaam na mikoani vijana wanaonekana kuhusudu jani la bangi utawakuta wamevaa mavazi au kama kofia,fulana, soksi , vilemba na hata kubandika picha za mmea wa bangi kwenye maeneo na shughuli mbalimbali wafanyazo.

Wanaziweka kwenye vioo na bodi za mabasi, taksi, bodaboda, vibanda vya biashara na kuvalia bangili mikononi zenye jani hilo.

Wanapozungumza wanaonyesha kupenda na kuvutiwa na jani hilo wakielezea namna ambavyo Marekani taifa kubwa linavyoruhusu matumizi ya mmea huo bila kificho.

Wanaamini kuwa Amerika imeona hauna madhara ndiyo maana unavutwa na kuna majimbo unatumiwa bila kikwazo.

Ni ukweli na hata mtandao wa US news, unataja majimbo zaidi ya 20 ya Marekani ambayo bangi inaruhusiwa kutumiwa kama burudani kisheria ambayo ni pamoja na Colorado, Washington, Alaska, Oregon, California, Nevada na Michigan na New York.

Aidha, kwa mujibu mtandao wa The National Institute on Drug Abuse (NIDA), wa nchi hiyo, unaporejea utafiti wa bangi uliofanyika Marekani, unasema kuwapo mabadiliko ambayo yameruhusu watu kuvuta bangi na kuihalalisha ni kiashiria kwamba inakubalika.

Mabadiliko katika sera za bangi katika baadhi ya majimbo kuihalalisha kwa matumizi ya matibabu au burudani ni wazi kuwa jani 'linakubalika' zaidi katika jamii hizo.

Mtandao huo unaonya kuwa ni muhimu sana watu kuelewa kile kinachojulikana kuhusu athari mbaya za kiafya zinazohusishwa na bangi.

Unasema kwa sababu bangi huharibu kumbukumbu na kukwamisha kufanya maamuzi tena inavuruga mtizamo ni hatari si kitu cha kuchekea.



> Robert anatoa mfano kuwa wafanyakazi wanakosa faraja na utulivu, pengine nyumbani, kazini na mitaani hivyo anaona hana namna wala kitu cha kumpa burudani na utulivu wa akili , ndiyo sababu anakimbilia kunywa pombe.

Jani hilo linaweza kuharibu utendaji kazi wa wanafunzi shuleni au watumishi kazini, jamii mitaani na kufanya iwe hatari zaidi kwa madereva wanaoendesha vyombo vya usafiri na usafirishaji.

Mtandao wa Nida unaitaja bangi kuwa ni hatari kwa kuwa huathiri mifumo ya ubongo ambayo kila wakati inaendelea kupevuka kuelekea utu uzima, kwa hivyo matumizi yake kwa vijana yanaweza kuwa na madhara mabaya na athari za kudumu katika ukuaji wao na fikra na utimamu kwenye kutambua na kuamua mambo.

Ripoti inaeleza kuwa mmea huo unawaweka watumiaji katika hasara na kuna uwezekano wa kuingilia ustawi wao kwa njia nyingine nyingi.

Nida inapinga imani maarufu kuwa bangi inapovuta inaleta kulewa na faraja na kuonya kuwa inaongeza changamoto za kiafya, akili na utimamu na shida zaidi za uraibu au uteja.

Iwapo kuvuta au kutumia bangi kuna manufaa ya kimatibabu ambayo yanazidi hatari zake za kiafya bado ni swali ambalo sayansi haijatatua, japokuwa majimbo mengi Marekani yanaruhusu kusambaza bangi kwa matibabu,

Kuna ushahidi mwingi kuhusu ufanisi unaotokana na bangi kitaalamu, lakini hata mamlaka za nchi hiyo za Kudhibiti Chakula na Dawa hazijaidhinisha "bangi kuvutwa kwa burudani"

Licha ya kwamba zipo dawa salama zinazotokana na kemikali za bangi na mmea wa bangi zilizopatikana kwa miongo kadhaa na zinaendelea kutumiwa, bado haiidhinishi matumizi ya jani hilo kwa burudani.

Hapa nchini hasa mijini vijana wengi wana mapenzi na mmea huo kwa mfano daladala zimebandikwa picha ya jani na inapewa majina na utukufu mwingi.

Kadhalika madereva, makondakta, waendesha pikipiki, bajaji, toyo na vyombo vingi vya usafiri huvalia vitambaa, kofia zenye mmea wa bangi au zilizoandikwa 'dope', fulana, vikuku mikononi na hata vidani shingoni vyenye picha ya bangi na katika hao wapo wengi wanaoivuta.

Bangi ina majina mengi kama wida, msuba, jani, kuku, ganja, weed na msokoto.

Kwa Tanzania bangi ni haramu lakini huenda inatumiwa na idadi kubwa ya watu licha ya kupigwa marufuku na kuharamishwa.

Roghat Robert, Mkurugenzi na muasisi wa Shirika la Akili Platform Tanzania, anasema mwaka 2022/23 alifanya utafiti wa kutambua sababu za vijana kutumia dawa za kulevya na katika majibu wanadai wanatafuta faraja.

Anasema vijana wengi wanadai wamevurugwa na kila wakati wanalazimika kutafuta faraja kwa wakiume na wanaume wajiingiza kwenye kubeti au kamari, dawa za kulevya, pombe kali, bangi na mirungi, lakini wapo wanakwenda kwenye kamari za gharama kubwa kwenye kasino hasa majijini.

Robert mbobezi wa masuala elimu maalumu kwa wenye mahitaji maalum na masuala ya saikolojia, anaongeza kuwa kadhalika kupendelea kutumia bangi kunatokana na kusaka faraja.

Anafafanua kuwa wanasaka kujifariji kwa muda huo , tena wanamini watafanyakazi yoyote, hata kama ni ngumu wataiona nyepesi.

"Ndivyo wanavyoaminishwa na wale waliowatangulia au wanaoitumia wakichukulia kuwa bangi inaweza kuwa tiba ya kutatua matatizo yao kwa wakati huo. Yote hayo yanatokea baada ya kufikia mwisho wa kufikiria."

Anaongeza kuwa suala la kusaka faraja si kwa wanaume pekee hata wanawake mabinti na watu wazima wapo wanaojiingiza kwenye biashara ya ngono usiku.

Wapo wengine wanaolewa kupindukia, kukataa ndoa, kuishi na familia wakitaka kukaa wenyewe na kufanya mambo wanayoyataka hata kama si sahihi kwa jamii, kama kuanzisha biashara za madanguro nakuuza dawa za kulevya, anasema.

Anaongeza kuwa vijana wengi wanapotea kutokana na kukosa malengo wengine hawana maarifa, lakini pia hofu ya Mungu wala ya watu na wanafanya mambo ambayo hayoko sawa.

"Kukosa faraja hata kazini asilimia kubwa ya wafanyakazi iwe sekta binafsi au umma wanajiingiza kwenye kusaka faraja mfano pombe, kulewa muda wote, kuwa na wapenzi wengi hata dawa za kulevya" anaeleza.

Robert anatoa mfano kuwa wafanyakazi wanakosa faraja na utulivu, pengine nyumbani, kazini na mitaani hivyo anaona hana namna wala kitu cha kumpa burudani na utulivu wa akili , ndiyo sababu anakimbilia kunywa pombe.

Anakumbusha kuwa Tanzania kuna msemo kuwa ukinywa pombe unapunguza mawazo, unajienjoy na inakupa burudani.

Anapendekeza kuwa ili kupata ufumbuzi wa tatizo hilo serikali irudishe masomo ya maadili na uongozi shuleni, vyuoni na makazini ili kuwafundisha watu kukabiliana na changamoto kama hizo zinawaingiza kwenye kutegemea vilevi na mambo yasiyo na maadili kupata faraja na burudani.



# Askofu aishauri CCM kumwongezea muda Samia

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MKUU wa Kanisa la Pentecostal Mountain of Prayers International Church Tanzania (PMPICT), Askofu Greda Lusinde, amekiomba Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutokuwa na mawazo ya kumsimamisha mgombea mwingine katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 zaidi ya Rais Samia Suluhu Hassan hata kama katiba yao inawaruhusu.

Askofu Lusinde, alisema hayo juzi alipokuwa akitoa ujumbe wa mwaka mpya wa 2024 kwenye ibada iliyofanyika makao makuu ya kanisa hilo Kikuyu Kusini mkoani hapa.

Katika ujumbe wake alikiomba CCM kutomsimamisha mgombea mwingine kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka 2025 , zaidi ya Rais aliyepo madarakani hivi sasa ambaye ni Samia Suluhu Hasaan.

Alisema ikiwa CCM watathubutu kufanya hivyo watakuwa na roho ya tamaa na kutamani madaraka ya uongozi kwa malengo ya kutaka kujinufahisha kwa baadhi ya watu tofauti ya hivi sasa ambapo kila mtanzania anafurahia nchi yake.

“Tunahitaji kumpa na kumchagua Samia Suluhu Hassan kwa sababu kibari cha Mungu alichompa kiti cha ufalme cha Ikulu hakikuwa batili bali ni mpango wa Mungu” alisema.

Aidha, alisema tangu amekuwa mtawala wa kiti hicho cha urais wameshuhudia Tanzania ikikua kiuchumi zaidi bila kujali itikadi yoyote ya siasa, chama, dini, rangi au kabila, wote wamekuwa wakifurahia matunda ya nchi yao.

Alisema hatakama Rais Samia anaupungufu ambao watanzania wanayaona hayo yapo kwa kila mwanadamu.

Kiongozi huyo wa kiroho pia aliwaomba viongozi wa dini kutokukubali vishawishi vyovyote vitakavyotolewa na nchi za Magharibi zinazoshabikia suala la ndoa za jinsia moja kwakuwa kitendo hicho ni dhambi kubwa mbele za Mungu.

“Kutokana na ukubwa wa dhambi hiyo tukumbuke kuwa Mungu aliuteketeza ulimwengu kwa Sodoma na Gomora kutokana na dhambi, hivyo tunatakiwa kuzilaani nchi ambazo zinazokubaliana juu ya mume kumuoa mwanamme mwezake” alisema

Awali akihubiri kwenye ibada hiyo aliwataka waumini wa kanisa hilo kuomba kwa gharama zote kwa ajili ya uchaguzi zitakazofanyika kuanzia wa serikali za mitaa na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Alisema kusudi la maombi hayo kwanza ukawe ni uchaguzi wenye amani na wakapatikane viongozi ambao watakaokuwa na hofu ya Mungu na wenye kujali masilahi ya Watanzania wote bila kujali itikadi.



Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu nchini (CWT), Japhet Maganga (kulia), akiwa na waalikwa wenzake kutoa maoni katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ambapo kamati hiyo imeanza kupokea maoni ya wadau mbalimbali kuhusu miswada minne ya sheria. Mikutano hiyo imeanza mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC awapa ujanja kuotesha miche kisasa

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri amewataka wadau wa mazingira wanaojishughulisha na uoteshaji miche ya miti kuacha kufanya kazi hiyo kwa mazoea, bali waitumie kama biashara itakayowaletea kipato na kujikwamua kiuchumi.

Aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na kikundi cha mazingira kiitwacho chapa kazi, wakazi wa Kata ya Dodoma Makulu na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) wakati wa upandaji miti, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya kutimiza miaka 20 ya kikundi hicho.

Akizungumza wakati wa upandaji miti hiyo kwenye eneo ambalo ofisi ya mkuu wa wilaya inatarajiwa kujengwa alisema vikundi vya uoteshaji miche ya miti vinapaswa kuitumia kazi hiyo kama biashara ili kujipatia kipato.

Hivyo, aliwataka wadau wa mazingira pamoja na malengo waliyojiwekea ya kuufanya mkoa kuwa wa kijani pia waelekeze kwenye kujiinua kiuchumi kwa kufanya biashara ya miche wanayozalisha.

“Ni wakati wenu sasa kujiwekea malengo kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi, pamoja na juhudi kubwa mnayoifanya ya kuuwezesha mkoa kuwa wa kijani pia msisahau kuwa na mtizamo wa kibiashara wa kuuza ndani na nje miche mnayozalisha”alisema.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Dodoma, Sakina Mbugi aliwataka Watanzania kuwa mabalozi wa kupanda miti na kuiliinda inayopandwa kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo katika majengo ya taasisi za serikali.

Alisema wadau wa mazingira na serikali wamekuwa na juhudi kubwa kuhakikisha upandaji miti unakuwa endelevu, hivyo wananchi wanatakiwa kuunga mkono juhudi hizo ili mkoa uweze kufikia malengo yake.

“Miti ni viumbe hai kama ilivyo kwa vingine, hivyo wakazi wa Dodoma tunatakiwa kushirikiana kwa pamoja na serikali na wadau mbalimbali wa mazingira katika kuotesha vitalu, kupanda na kuituza na hatimaye tufikie malengo yetu,” alisema.

Pia alikishauri kikundi cha chapa kazi kuwa shamba darasa kwa wadau wengine kutokana na juhudi kubwa wanazozifanya za kueneza elimu ya umuhimu wakupanda miti.

Katibu wa kikundi hicho, Marco Malongo, alisema kwa miaka 20 waliyofikisha wamesaidia kwa kiasi kusambaza miti na kuufanya Mkoa wa Dodoma kuwa wa kijani.

Alisema juhudi hizo ni pamoja na uoteshaji na usambazaji wa miche ya miti kwenye maeneo mbalimbali ya matunda na kivuli.

Malongo alisema kikundi hicho kitahakikisha kinashirikiana na serikali pamoja na wadau wa mazingira na wananchi ili upandaji miti uwe endelevu na kuwa tabia ya kila mwananchi kupenda kupanda mti wa matunda na kivuli kwenye eneo lake analoishi

# Makamu Mkuu UDOM ateta na ujumbe kutoka Marekani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Prof. Lughano Kusiluka, amefanya mazungumzo na ujumbe kutoka Chuo Kikuu cha Uuguzi Rutgers cha Marekani.

Chuo hicho ni wadau wa maendeleo na UDOM kupitia Shule Kuu ya Uuguzi na Afya ya Jamii.

Akikaribisha ujumbe huo, Prof. Kusiluka ameelezea shukrani zake kwa ushirikiano na ufadhili unaotolewa na Chuo Kikuu cha Rutgers kwa Shule Kuu ya Uuguzi na Afya ya Jamii ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Alisema matarajio makubwa ya UDOM ni kuendeleza na kuanzisha miradi mingi zaidi ya kujifunza na ufundishaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha kozi mpya za uuguzi na afya ya jamii.

“Kwa kuzingatia ongezeko la matumizi ya teknolojia nchini na uwekezaji mkubwa tulioufanya katika miundombinu ya TEHAMA, sioni sababu ya kutokufundisha baadhi ya programu kwa njia ya masafa kwa kushirikiana na wataalamu wenzetu waliopo Rutgers” alisema Prof. Kusiluka.

Aidha aliwataka viongozi wa Shule Kuu ya Uuguzi na Afya ya Jamii, kutumia fursa zilizopo katika kuanzisha kozi ambazo zitakuwa na manufaa kwa taifa na zinazoweza kufundishwa kupitia mtandao.

Akizungumza kwa niaba ya ujumbe kutoka Chuo Kikuu cha Rutgers, Dk. Emilia Iwk, alieleza kuwa kupitia ushirikiano uliopo kati ya vyuo hivyo viwili, wamepanga kuongeza maeneo ya ushirikiano ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wataalamu wa UDOM, ili kuongeza ujuzi na kupanua wigo wa mafunzo kwa wanachuo.

Kwa sasa UDOM kina ushirikiano na Chuo Kikuu cha Rutgers katika maeneo ya uandishi wa miradi ya pamoja ya utafiti, ufundishaji, ubunifu na kubuni mitaala mipya ya masomo.

Ujumbe kutoka Chuo Kikuu cha Rutgers uliongozwa na Dk. Emilia Iwk, akifuatana na viongozi wengine Dk. Antony Fillipelli na Catie Filippeli Apn, pamoja na wanafunzi 12 wanaosoma katika chuo hicho ambao wamekuja kujifunza na kubadilishana uzoefu na wanafunzi wenzao katika Shule Kuu ya Uuguzi na Tiba ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mkuu wa Idara ya “Clinical Nursing” ya UDOM, Angelina Alphonce Joho, alisema ujumbe huo utakuwepo nchini kwa majuma kadhaa.





# Serikali yaboresha upatikanaji elimu Chunya

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANAFUNZI wanaojiunga na masomo ya sekondari katika Kata ya Kambikatoto wilayani Chunya, wameondokana na adha ya kutembea umbali mrefu baada ya serikali kukamilisha ujenzi wa shule nyingine ya sekondari ndani ya kata yao.

Wanafunzi wao walikuwa wakisafiri umbali wa zaidi ya kilomita 110 kwenda kusoma katika shule jirani ya Lupatingatinga, hali iliyokuwa inasababisha utoro na wengine kutofaulu masomo yao.

Ujenzi wa shule hiyo umekamilika kwa kiwango ambacho kinaruhusu wanafunzi kuanza masomo kuanzia mwaka huu na tayari wanafunzi wameshachaguliwa kwenda kuanza kidato cha kwanza katika shule hiyo.

Mbunge wa Mbarali, Masache Kasaka, alitembelea shule hiyo na kusema kuwa vyumba vinane vya madarasa, ofisi za walimu na maabara mbili ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 100.

"Tunaishukuru serikali kwa kutupatia zaidi ya Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa shule hii ambayo kwa kweli ni msaada mkubwa kwa wananchi wangu," alisema Masache.

Alisema kuwa kuanza kwa shule hiyo ni mkombozi mkubwa kwa wazazi wa wanafunzi wa kata hiyo ambao kwa muda mrefu walikuwa na kero ya kusafirisha watoto wao kwenda shule za jirani na kutumia gharama kubwa kuwapangia vyumba vya kuishi wakiwa masomoni.

Baadhi ya wazazi wa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hiyo walisema uwapo wa shule hiyo umepunguza gharama kubwa za kuwasomesha watoto wao katika shule za sekondari ambazo zipo mbali na makazi yao.

Mkazi wa Kata ya Kambikatoto, Branditi Chingwile, baadhi ya wazazi walilazimika kuwashawishi watoto wasifanye vizuri mtihani wao wa darasa la saba ili wasifaulu ili kuepuka gharama za kusomesha.

Alisema kuwa pia wanafunzi ambao walitakiwa kwenda kusoma sekondari za jirani waliondoka kwa wazazi wao wakiwa na tabia njema lakini wakifika shuleni ambako walilazimika kuishi huko bila wazazi walijifunza tabia za ovyo jambo ambalo pia liliwakatisha tamaa wazazi kuwaruhusu watoto kwenda kusoma sekondari.

"Kero ya kukosa shule ya sekondari kwenye kata yetu ilikuwa na athari kubwa kwetu, wazazi tuliogopa kuwapeleka watoto shuleni kutokana na mambo mengi kwanza mazingira yalikuwa magumu kwa watoto, walijifunza tabia mbaya na pia gharama za kuwasomesha zilikuwa kubwa mmno," alisema Branditi.

Akisoma taarifa ya ujenzi wa shule hiyo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kambikatoto, Nicholous Ndogosya, alisema vyumba vinane vya madarasa, ofisi mbili, jengo la utawala na maabara mbili zimekamilika.

Alisema mbali na ujenzi wa shule hiyo ya sekondari, kata hiyo pia imekalisha ujenzi wa shule tatu za msingi na shule moja shikizi.

Alisema Shule mpya Sekondari ya Kambikatoto itakuwa ikipokea wanafunzi kutoka katika shule zote za msingi ndani ya kata hiyo ambazo kwa sasa zina jumla ya wanafunzi 20,590.



Baadhi ya wazazi wakinunua vitabu kwa mjasiriamali kwenye Soko la Tarafani katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki, yakiwa ni maandalizi ya kupeleka watoto wao shule. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mradi Liganga kuondoa adha kuagiza chuma nje ya nchi

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

IMEELEZWA kuwa mradi wa uchimbaji chuma wa Liganga utakapoanza utasaidia Tanzania kuondokana na adha ya kuagiza bidhaa za chuma ikiwamo nondo kutoka nje ya nchi kwa kuwa itazalishwa hapa nchini.

Hayo yalielezwa na Meneja Miradi ya Liganga na Mchuchuma kutoka Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC), Dk. Witness Ishuza, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya ziara ya Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Pindi Chana mkoani hapa.

Alisema kuwa katika eneo la Liganga wanategemea kuwa na mgodi wa chuma pamoja na kiwanda cha kuchenjua chuma ili kutengeneza bidhaa za chuma.

"Mradi huu ukianza tunapanga kila mwaka kuchenjua kupata chuma kiasi cha tani milioni moja, ambapo tutatengeneza bidhaa za chuma ambazo ni nondo, kuna flatbar, bidhaa zote za chuma ambazo tumezoea kuzinunua kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali," alisema Dk. Ishuza.

Pia alitoa rai kwa wananchi wanaozungukwa mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma kufanya uwekezaji wa aina mbalimbali ikiwemo kufuga ng'ombe wa maziwa kwa sababu uchimbaji utakapoanza kutakuwa na vumbi jingi.

"Kwa hiyo watu wawekeze kwenye kufuga ng'ombe wa maziwa ili wakati ukifika maziwa yapatikane mahali hapa sio wakati unafika alafu tunachukuwa maziwa sehemu nyingine," alisema.

Kwa upande wake, Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi DK. Pindi Chana alisema baada ya kutembelea eneo la Liganga amegundua kuwa chuma kipo cha kutosha.

"Ukiangalia ule mlima wote ni chuma, tunachuma cha kutosha tayari wananchi wameshalipwa fidia Sh. bilioni 15.4 tunashukuru sana serikali," alisema Dk. Chana.

Alisema kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, wanaangalia utajiri huo ikiwamo utajiri asilia na maliasili zilizopo nchini na kuona namna gani Watanzania wanakwenda kunufaika.

Alisema ziara hiyo ililenga kuangalia utaratibu na masuala yote na mikakati ambayo inakwenda kuwekwa kuanzia ngazi ya halmashauri hadi ngazi ya mkoa sambamba na kuangalia maeneo yote ambayo kuna maliasilia ili kujipanga kwa kushirikiana na watu binafsi.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ludewa, Stanley Kolimba, alitoa rai kwa wananchi ambao wamelipwa fidia kuwekeza katika miradi mbalimbali badala ya kuzitumia kwa matumizi yasiyokuwa na tija.

Kolimba aliiomba serikali kuharakisha kuanza kwa mradi huo mapema zaidi ili wananchi wanufaike na fursa ambazo zinatajwa.

## Wakulima walia uhaba wa mbegu za mahindi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MIKOA ya Nyanda za Juu Kusini imekumbwa na uhaba wa mbegu za mahindi, hali ambayo imesababisha wakulima kutoka maeneo mbalimbali kuzunguka katika maduka ya pembejeo jijini Mbeya kusaka mbegu hizo bila mafanikio.

Nipashe limeshuhudia wakulima wakipita kwenye maduka ya pembejeo jijini Mbeya wakitafuta mbegu za mahindi lakini wakiambulia patupu na kuishia kulalamika.

Julias Mapunda ambaye ni mkulima kutoka Songea mkoani, Ruvuma alisema amekosa mbegu za mahindi mjini Songea, hali iliyomlazimu kusafiri hadi Makambako mkoani Njombe ambako pia hakufanikiwa kuzipata na ndipo akaamua kwenda Mbeya akidhani atazipata.

"Baada ya kukosa mbegu Songea nilikwenda Makambako ambako nilizunguka kwenye maduka karibu yote kutafuta mbegu nikakosa ndipo nikaamua kuja Mbeya, nilipofika Mbeya nashangaa kukutana na wakulima wenzangu wengi tukiwa na tatizo linalofanana, kwa kweli mbegu zimeadimika na hii inatukosesha amani kwa sababu msimu wa kupanda ndio unakaribia kuisha," alisema Julius.

Rukia Mwanibanza yeye ni mkulima wa mahindi kutoka Mbozi, mkoani Songwe, alisema jitihada zake za kusaka mbegu katika miji ya Tunduma, Vwawa na Mlowo mkoani Songwe ziligonga Mwamba na ndipo akaamua kuelekea Mbeya akidhani atapata mbegu.

"Nilipoamua kuja Mbeya nilishuka Mbalizi, nikazunguka kwenye maduka ya pembejeo kutafuta mbegu nikakosa, ndipo nikaamua kuja hapa Mwanjelwa ambako pia nimezikosa," alisema Rukia.

Akizungumzia suala la uhaba wa mbegu, Mkurugenzi wa Kampuni ya uzalishaji wa Mbegu za Panna, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Elias Torio, alikiri kuwapo kwa uhaba wa mbegu katika kipindi hicho.

Alisema uhaba huo wa mbegu umesababishwa na mazingira mazuri ya kilimo ambayo yamewekwa na serikali na kusababisha mwamko mkubwa wa wakulima kuingia shambani hali ambayo haikuendana na makadirio yao ya uingizaji wa mbegu.

Hata hivyo alisema kuna shenena ya mbegu imeagizwa na itawasili muda wowote kuanzia sasa na kumaliza kabisa kero hiyo kwenye mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini.





# Dk. Mwinyi: Mapinduzi yamefungua fursa elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema Mapinduzi ya 1964 yamefungua fursa za huduma za maendeleo ya kiuchumi na kijamii Zanzibar, ikiwamo elimu ambayo sasa inapatikana bure.

Alisema kupitia Mapinduzi serikali iliyoongozwa na Hayati Mzee Abeid Aman Karume, ilitangaza elimu bure kwa wananchi wote na kuifanya kuwa ni haki ya msingi ya kila raia.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua shule ya msingi Fuoni Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, ikiwa ni mwendelezo wa shamrashara za miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema Serikali ya Zanzibar inaendelea na mikakati ya kuifanyia sekta ya elimu mageuzi makubwa ili kuiimarisha iwasaidie vijana kumudu maisha yao na kupata wataalamu wanaohitajika kwa maendeleo ya nchi.

Alisema mageuzi hayo yamezingatia kuimarisha miundombinu ya elimu, kuimarisha uongozi na wa maendeleo ya elimu katika ngazi zote ikiwamo kuanzisha tume ya walimu kwa ajili ya kusimamia masuala ya walimu na mitaala.

Alisema pia wamelenga kuimarisha vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuimarisha matumizi ya teknolojia katika elimu ili watoto wapate elimu bora. "Utekelezaji wa mageuzi haya tayari umeanza na utaendelea kwa awamu. Jumla ya shule 25 za ghorofa zinajengwa Unguja na Pemba katika mwaka huu wa fedha wa 2023/2024 pekee ikiwemo shule hii ya ghorofa mbili hapa Fuoni. Shule hii tunaifungua leo na nyingine zitakamilika na kufunguliwa mapema mwaka huu," alisema.

Aidha, alisema lazima watoto kuandikishwa shule, kukamilisha elimu yao ya msingi na kuendelea na masomo yao katika ngazi nyingine zinazofuata na hatimaye kufanikiwa kujiunga elimu ya vyuo vikuu ili nchi ipate wataalamu wake wenyewe na kupiga hatua kubwa zaidi za maendeleo.

Dk Mwinyi alisema kufanya hivyo ni kuyaenzi Mapinduzi na kuitendea haki Serikali ambayo imefanya juhudi kubwa kuhakikisha inaimarisha huduma za elimu kote nchini.

Katibu mkuu wizara ya elimu na mafunzo ya amali Zanzibar, Khamis Abdallah Said, alisema ujenzi wa shule hiyo ya msingi ya Fuoni umetokana na changamoto wanazozipata watoto wa eneo hilo za uhaba wa madarasa unaosobabisha msongamano mkubwa wa wanafunzi wenye wastani wa wanafunzi 80 kwa darasa na pia shule kuendeshwa kwa mtindo wa mikondo miwili.

Alisema ujenzi wa shule hiyo mpya inajengwa kwa fedha za Serikali ya Zanzibar ambapo jumla ya Sh. 7,826,106,000 zimetumika mpaka kukamilika kwake.

"Shule hii imejengwa na kampuni ya ROK Development B.V ya Uturuki na kusimamiwa na Wakala wa Majengo ya Serikali (ZBA). Ujenzi wa Shule hii ulianza rasmi mwezi Mei mwaka 2023 na kumalizika mwezi wa Disemba, 2023. Mheshimiwa Rais, na leo hii Januari, 7, mwaka 2024 unaifungua rasmi ikiwa ipo tayari kutumika,"alisema.

Alisema ujenzi wa Shule hiyo ni ya ghorofa umetumia teknolojia ya PRE Fabricate inayopunguza uharibifu wa mazingira kwa kutumia mchanga kidogo ambayo haijawahi kutumika katika ujenzi wowote wa shule za Zanzibar.

Alisema jengo hilo na lina madarasa 29, vyoo 24, afisi moja ya mwalimu mkuu na tatu za walimu, ukumbi mmoja wa kufanyia mitihani, maabara moja , chumba kimoja cha TEHAMA, Maktaba moja na stoo mbili.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (wa pili kulia), akifunua kitambaa kuashiria ufunguzi wa jengo la Mamlaka ya Maji Zanzibar, wilayani Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi jana. Wa nne kushoto ni Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Shaibu Kaduara. **PICHA: OFISI YA NAIBU WAZIRI MKUU**

# Biteko ataka uaminifu miradi ya maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Tanzania, Dk. Doto Biteko, amewataka wanaopewa nafasi za kusimamia miradi ya maendeleo wawe waaminifu ili wananchi waondokane na matatizo yanayowakabili.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua Ofisi mpya ya Mamlaka ya Maji (ZAWA) zilizopo Mtaa wa Muembe Madaema visiwani humo.

Alisema wananchi wanategemea kupata huduma ya majisafi na salama katika shughuli zao za kila siku hivyo ufunguzi wa mradi huo, utaondosha tatizo la maji.

"Ni vyema kuwahudumia wananchi kwa kuwapatia miradi mbalimbali hasa ya maji na maji ni miongoni mwa huduma muhimu katika nchi," alisema Biteko.

Akitoa taarifa ya kitaalamu, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar, Dk Salha Mhamed Kassim, alisema kuwa ujenzi huo umegharimu dola za milioni 92 .8 chini ya usimamizi wa Mamlaka hiyo.

Aidha alisema kuwa mradi huo umegawanyika katika sehemu tatu ikiwemo mradi wa matangi ya maji yaliyopo Mkorogo pamoja na mradi wa Skimu ya Masingini ikiwemo ujezi wa Ofisi hiyo.

Waziri wa Maji Nishati na Madini Shaibu Hassan Kaduara, alisema Zanzibar, imepiga hatua kubwa ya kusambaza huduma ya maji safi na umeme katika maeneo mengi ya Unguna na Pemba.

Aidha alisema kuwa wanatarajia kujenga miradi mikubwa 25 katika Mkoa Ukusini Unguja na kuwaomba wananchi kuendelea kuchangia Maji ili kuimarisha miundombinu idumu kwa muda mrefu.

# Serikali kujenga hospitali ya kisasa kisiwani Tumbatu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, amesema serikali inatarajia kujenga hospitali mpya ya kisasa katika kisiwa cha Tumbatu ambayo itakuwa inatoa huduma zote muhimu ikiwamo za uzazi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kufuatia wakazi wa kijiji cha Jongowe kisiwani huko kulalamikia kutokuwa na huduma ya uzazi licha ya kuwa na zahanati inayotoa huduma za afya ngazi ya msingi.

Alisema katika kisiwa hichi chenye watu 25,000 kuna vituo viwili vya afya katika vijiji vya Jongowe kisicho na huduma ya uzazi na cha Kichangani ambacho kinatoa hiyo kwa akinamama wanaotaka kujifungua.

Alisema kukosekana kwa huduma za kujifungua huwalazimu kuvuka bahari kwenda hospitali ya Kivunge na wengine kujifungua kwa wakunga wa jadi jambo ambalo ni hatari kwa afya ya mama na mtoto.

"Tumbatu kuna vituo viwili vya afya Jongowe na Kichangani lengo letu ni kujenga hospitali kubwa ambayo itajengwa baina ya Kichangani na Jongowe ili kila upate kuwarahisishia kufika hospitalini hapo kupata huduma," alisema.

Alisema hospitali hiyo inayotarajiwa kuanza kujengwa Machi, mwaka huu itakuwa na uwezo wa kulaza wagonjwa 25 kwa wakati mmoja, itatoa huduma za uzazi kwa njia ya kawaida na upasuaji na itakuwa na wataalamu wa kutosha.

Alisema serikali itahakikisha inajenga hospitali zinazotoa huduma za uzazi katika visiwa vyote vidogo vinavyoishi watu Unguja na Pemba ili kuokoa maisha ya mama na mtoto wakati wa kujifungua na kuwaondoshea usumbufu wananchi kufuata huduma hizo nje ya visiwa hivyo.

Hata hiyo Mazrui alisema lengo la serikali kujenga hospitali mpya kila wilaya ili kupunguza mrundikano wa wagonjwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja lakini bado idadi ya wagonjwa haipungui na hospitali mpya zimefurika wagonjwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAVIS YUSUPH SEMUGURUKA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4867/0040/2016 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KITUNGWA ADVENTIST SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/MWA/NYA/9316/2023**

## CHETI CHA CHUO KIKUU KIMEPOTEA



Ndugu **EPHRAIM MWANGOMO** anatangaza kupotea kwa cheti chake cha Chuo kikuu, kilichotolewa na **CHUO KIKUU CHA DAR-ES-SALAAM** mwaka 1997. Kwa yeyote atakayekiona anaombwa atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu.

**Taarifa Polisi: PHQ/DAR/KIN/2587/2024.**

## VYETI VIMEPOTEA



Ndugu **EPHRAIM MWANGOMO** anatangaza kupotelewa na vyeti vyake Elimu ya Secondary ambavyo ni kidato cha Nne chenye Index No: **S.0434-050** shule ya Ndembela Secondary School, kilichotolewa na Baraza la Mitihani 1990. Na cheti cha Kidato cha 6 chenye Index **No: S.0153-590** Songea Boys Secondary School kilichotolewa **1993.** Kwa yeyote atakayeviona anaombwa kutoa taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu.

**Taarifa Polisi:PHQ/DAR/KIN/2585/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**EMANUEL P. MWAGALA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2121-0097 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia LUHUNGA SECONDARY SCHOOL mwaka 2013 na cheti cha chuo chenye usajili namba EQ643-0071 kilichotolewa na chuo cha RUNGEMBA mwaka 2016. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.


**POLISI TAARIFA: PHQ/MAR/MUS/2355/2023**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE OATH (JUDICIAL PROCEEDINGS) AND STATUTORY DECLARATION**
**ACT, 1966 (R.E 2019)**
**DEED POLL**

BY THIS DEED, I MURSHIDI RASHIDI KAIZA , an adult moslem of Dar es salaam, do hereby renounce the names of MURSHIDI RASHIDI as my names, and in lieu thereof do assume and adopt the name of MURSHIDI RASHIDI KAIZA.

AND IN PURSUANCE of such change of name as aforesaid, I DO HEREBY DECLARE THAT, I shall at all times here after in all records, deeds and instruments in writing and in all actions, proceedings and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever, use and sign the said name of MURSHIDI RASHIDI KAIZA as aforesaid.

AND I HEREBY AUTHORISE and request all persons and authorities to designate and address me, in the name of **MURSHIDI RASHIDI KAIZA only. IN WITNESS WHEREOF** I have hereunto subscribed my name MURSHIDI RASHIDI KAIZA on the date and manner hereunder appearing:



SIGNED and DELIVERED at Dar es Salaam
by the said MURSHIDI RASHIDI KAIZA
who is known to me personally /
identified to me by......
the latter being known to me personally
in my presence on this 6th day of December 2023

DEPONENT

BEFORE ME:
Signature: ......
Postal Address: P. O. Box, 22363, Dar es Salaam
Qualification: ADVOCATE/COMMISSIONER FOR OATHS

**UNCLE MO ENTERPRISES**
**Dealing with court/tribunal broker, auction, debit collection etc**
**P.O. BOX 43 DODOMA, Email:morisndomba@gmail.com**
**Tel:+255717417520 +255765684345**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini niliyopewa na MAHAKAMA YA MWANZO DODOMA MJINI tutakuwa na mnada kiwanja chenye nyumba kilichopo MBUYUNI, mali ya mdaiwa BARAKA SADICK KAFUMBA ambaye ni mdaiwa kwa ACHASE FINANCE (T) LTD. Mnada utafanyika tarehe 12/01/2024 Mbuyuni kata ya kizota.

**MASHARTI YA MNADA**

- Wanunuzi wataruhusiwa kukagua nyumba siku hiyo hiyo yam nada
- Mnunuzi atakayefika bei ya kununua nyumba atawajibika kulipia asilimia 25% za mauzo papo kwa hapo na kiasi kinachobakia atatakiwa kulipia ndani ya muda wa siku 14 toka malipo ya kwanza,
- Mnunuzi atawajibika kuchukua mali/kukabidhiwa mpaka atrakapomaliza malipo yote ya manunuzi.

**ILANI ATASKAYECHEZEA MNADA ATACHUKULIWA HATUA ZA KISHERIA. KWA MAWASILIANO 0717417520, 0717073423, 0766170811**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO .157/2023**

**In the matter of the Estate of the late FOIBE MSAMBAZI MNYANGULU of Matumbulu within Dodoma**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY PETER IVAN MUHETA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are here by cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant o letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 16 Day of 1, 2024

Dated at Dodoma this 4 Day of 1, 2024




**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Kenya yaiomba Tanzania msaada dawa za TB

**NAIROBI,** KENYA

WAZIRI wa Afya wa Kenya Wafula Khumicha amesema kuwa nchi yake inatafuta msaada wa Tanzania ili kukabiliana na uhaba wa dawa za Kifua Kikuu.

Waziri huyo alisema jana kuwa Kenya imekumbwa na uhaba wa dawa hizo tangu Oktoba mwaka jana na imeweka hatua za kuhakikisha ugavi usioisha kwa hospitali za serikali ikiwa ni pamoja na mabadiliko kutoka kwa mgavi mmoja hadi wasambazaji wengi.

"Mwishoni mwa Septemba na Oktoba mwaka jana tulikuwa na uhaba wa dawa za Kifua Kikuu, lakini tulijitahidi kwa kiasi ambacho tulipata msaada kutoka nchi jirani ya Tanzania na tulipata akiba ya kutosha ambayo sasa imesambazwa," alisema.

Aliongeza kuwa serikali inajitahidi kuhakikisha kuwa hifadhi yake ya dawa za matibabu ni ya kutosha ili kuhakikisha hakuna mgonjwa anayekosa dawa zake. Na kwamba hadi mwisho wa Januari, hospitali zote za umma nchini humo zitakuwa zimepokea dawa hizo.

"Pia tumefanyia kazi mnyororo wetu wa ugavi na tunatarajia kwamba hivi sasa hisa zinapaswa kuwa sawa na tutakuwa tukipokea hifadhi zaidi ifikapo Februari ili kuhakikisha kuwa wagonjwa wanahudumiwa," alisema.

## Mashambulizi yawaondoa wahudumu wa afya Gaza

**GAZA,** PALESTINA

MASHIRIKA ya kimataifa ya misaada ya kimatibabu yamesema kuwa kuongezeka kwa shughuli za kijeshi za Israel kumewafanya wahudumu wa afya kulazimika kuacha kufanya kazi katika hospitali ya al-Aqsa mjini Gaza.

Katika taarifa iliyotolewa jana na timu ya matibabu ya dharura ya Wapalestina na Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji (EMT) ilisema jeshi la Israel limetupa vipeperushi vinavyotaja maeneo yanayozunguka hospitali hiyo kama eneo hatari, na kuongeza kuwa kutokana na historia ya Israel ya mashambulizi dhidi ya wafanyakazi wa afya na vituo vya afya huko Gaza wahudumu wa afya hawawezi kurudi.

Profesa Nick Maynard, ambaye ni daktari wa upasuaji na kiongozi wa kliniki EMT, alisema idadi ya majeruhi waliletwa hospitalini katika siku chache zilizopita imekuwa ya kutisha.

Dk. James Smith, mtaalam wa matibabu ya dharura na EMT, alisema "Nahofia usalama wa watu katika eneo hilo, wafanyakazi wa Palestina ambao tumefanya kazi pamoja, mamia ya wagonjwa hospitalini, na maelfu ya watu waliohamishwa katika eneo hilo. hospitali na kambi za karibu". **BBC**

# Mahakama DRC kusikiliza kesi kuhusu uchaguzi mkuu

**KINSHASA,** DRC

MAHAKAMA ya katiba nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo imeanza kusikiliza kesi kuhusu uchaguzi mkuu uliomrudisha tena madarakani Rais Felix Tshisekedi.

Kesi hiyo inaanza huku viongozi wa upinzani wakiendelea kusisitiza matakwa yao ya kufutwa kwa ujumla uchaguzi huo uliofanyika Disemba 20, 2023 wakitoa hoja kwamba, ulifanyika udanganyifu.

Hayo yalijiri baada ya Tume Huru ya Uchaguzi (CENI), kufuta matokeo ya wagombea 82 katika uchaguzi wa ubunge wa kitaifa na ule wa mikoa kwa tuhuma za udanganyifu, ufisadi na umiliki haramu wa vifaa vya kupigia kura.

Ilielezwa kuwa ni Wakongo wawili ndio waliwahi kufikisha malalamiko yao mbele ya mahakama ya katiba ambao ni Théodore Ngoy ambaye ni miongoni mwa waliogombea kiti cha urais pamoja na mwananchi mwingine mmoja wa kawaida.

Baadhi ya wagombea wengine wa urais wakiwemo Moïse Katumbi, Martin Fayulu na Denis Mukwege nao wametaka matokeo ya uchaguzi yabatilishwe japokuwa walikataa kufikisha malalamiko yao mbele ya mahakama ambayo wanaamini ni ya kikabila na inatumiwa na jamii ya Raïs Félix Tshisekedi.

Wagombea wanane wanaamini kuwa kasoro zote zilifanyika katika ushirikiano na utawala wa Tshisekedi, kama alivyoeleza Martin Fayulu, "Tumetambua kwamba walionufaika na vifaa vya kupigia kura wote ni kutoka familia moja ya kisiasa, ya Tshisekedi".

"Sasa CENI itaonyesha vipi kuwa katika uchaguzi wa pamoja, ni uchaguzi wa wabunge tu ndio uliibiwa ila sio ule wa rais," alihoji.

Dieudonné Mushagalusa, mratibu wa muungano huo alisema "Tunaendelea kusema chaguzi zote hizi zifutwe ili kuziandaa upya katika utaratibu. Hivi CENI tayari imekiri kila kitu tulichokuwa tumekionya. Tunatarajia sasa mahakama ya katiba kuahirisha uthibitisho wa matokeo ya mwisho ya mgombea yoyote".

**DW**



Mmoja wa wapinzani Prince Epenge akiongea na waandishi wa habari wakati wa maandamano ya kushinikiza kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi wa Desemba 20 mjini Kinshasa, juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Polisi waliovuruga sherehe ya Odinga kuadhibiwa

**NAIROBI,** KENYA

INSPEKTA Jenerali wa Polisi nchini Kenya (IG) Japhet Koome, ameapa kuchukua hatua kali dhidi ya maofisa wa polisi waliovuruga sherehe ya kuzaliwa ya kiongozi mkuu wa upinzani nchini humo Raila Odinga.

Inaelezwa kuwa juzi maofisa wa polisi walirushia vitoa machozi wafuasi wa Odinga, waliokuwa wamekusanyika karibu na Nairobi Archives kwa hafla ya kukata keki.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na inspekta huyo jana, hatua za kiutawala zitachukuliwa dhidi ya maofisa waliowarushia vitoa machozi wafuasi wa Raila waliokuwa wamekusanyika katika Hifadhi ya Kitaifa kusherehekea miaka 79 ya kuzaliwa kwa kiongozi huyo wa ODM.

Pia IG Koome alisema kitendo hicho cha polisi hakikuwa na msingi kwani wafuasi wa Raila walikuwa wakiandaa sherehe ya amani pekee.

"Huduma ya Kitaifa ya Polisi inatambua mtawanyiko wa ghasia usio na msingi wa wananchi waliokuwa wakifanya sherehe za amani jijini Nairobi. Hatua kali za kiutawala zichukuliwe dhidi ya maofisa waliohusika na kitendo hicho kinyume cha sheria," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Aliongeza kuwa huduma ya kitaifa ya polisi imejitolea kutoegemea upande wowote wa kisiasa wakati wa kutekeleza majukumu yake.

"Huduma ya Kitaifa ya Polisi inasisitiza dhamira yake ya kutoegemea upande wowote wa kisiasa katika kutekeleza jukumu lake la kulinda maisha na mali," ilisema taarifa hiyo.

Aidha, viongozi wanaounga mkono Chama cha Muungano wa Azimio la Umoja One Kenya na Wakenya wengine walijitokeza kwenye mitandao ya kijamii kulaani kitendo hicho cha polisi.

Mbunge wa Westlands Tim Wanyonyi alisema serikali ina hofu kwa sababu Wakenya wana hasira na utawala wa Rais William Ruto.

"Polisi walijitokeza na kuwarushia vitoa machozi wafuasi wetu. Serikali ina hofu kwa sababu ya mvutano na Wakenya ambao hawana pesa shule zikifunguliwa," alisema.

**KTN**

# SIMBA QUEENS, JKT QUEENS MECHI KALI YA MAAMUZI LEO

**Na Saada Akida**

WAKATI nyasi za viwanja vitatu kwa upande wa soka la wanawake zikitarajiwa kuwaka moto leo, macho na masikio yatakuwa katika Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, kushuhudia mabingwa watetezi wa ligi hiyo, JKT Queens wakiwakaribisha mabingwa wa Ngao ya Jamii, Simba Queens.

Michezo mingine miwili itakayopigwa leo ni kati ya wenyeji, Baobab Queens dhidi ya Geita Gold Queens katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma na Amani Queens dhidi ya Alliance Girls kwenye Dimba la Ilulu mkoani Lindi.

Pamoja na kuwapo kwa michezo hiyo, lakini mechi kati ya JKT Queens dhidi ya Simba Queens inanavuta zaidi hisia za mashabiki kutokana na ubora wa timu hizo na ushindani zinapokutana.

Hata hivyo, mchezo huo unatarajiwa pia kuwa wa maamuzi wa timu ipi itakaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kwa tofauti ya ponti kwani hadi sasa zote zina alama tisa kutokana na michezo mitatu kila moja iliyocheza, lakini JKT Queens yenyewe inaongoza ligi hiyo kutokana na idadi kubwa ya mabao. JKT Queens hadi sasa ina mabao 15 huku ikiwa haijaruhusu nyavu zake kutikishwa, wakati Simba Queens imecheka na nyavu mara 13 na ikiruhusu kipa wake kugeuka kuokota mpira nyavuni mara tatu.

Timu hizo zinakutana kwa mara ya pili msimu huu, baada ya mwezi uliopita kukutana katika fainali ya Ngao ya Jamii, Simba Queens ikiibuka na ubingwa kwa kumfunga JKT Queens kwa mikwaju ya penalti 5-4 baada ya dakika 90 kumalizika kwa sare ya bao 1-1.

Kuelekea mchezo huo Kocha Mkuu wa JKT Queens, Esther Chabruma, amesema kikosi chao kipo tayari kwa mechi hiyo na kutafuta pointi tatu muhimu dhidi ya Simba Queens.

Alisema haitakuwa mechi rahisi kwa sababu ya ubora wa timu zote mbili, lakini wamefanya maandalizi mazuri kuhakikisha wanafanikiwa kupata matokeo chanya katika uwanja wao wa nyumbani.

"Ni mchezo muhimu sana kwetu, tumefanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi tulizocheza licha ya kushinda, lakini kuna makosa tumefanya na tayari tumesahihisha na kuongeza vitu kwenye ubora wetu, wachezaji wangu wako tayari kwa mchezo huo wa kesho (leo)," alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Juma Mgunda, kwa upande wake amesema maandalizi yameenda vizuri na itakuwa mechi nzuri na wachezaji wapo tayari kwa ajili ya kupambana na kusaka alama muhimu ili kufikia malengo yao.

Alisema licha ya kupata ushindi katika michezo mitatu waliyocheza na kushinda, aliona mapungufu na wameyafanyia kazi kwa kusahihisha makosa yao na kuongeza ubora kwenye ubora wao.

"Malengo yetu ni mwisho wa msimu kutwaa ubingwa na kurejesha heshima ya klabu. Itatulazimu tucheze vizuri na kushinda katika mechi zote ikiwamo mechi yetu ya kesho (leo) dhidi ya JKT Queens.

Ni timu nzuri na wana wachezaji wazuri, tutaingia na mbinu tofauti katika mchezo huu, tunahitaji kupata alama muhimu katika mchezo huu dhidi ya wapinzani wetu wakubwa," alisema Mgunda.

**KITASA...**



Kocha Msaidizi wa Simba, Farid Zemit (kulia) na Kocha wa Viungo, Kamal Boudjenane, wakimtazama kiungo mkabaji mpya wa timu hiyo, Babacar Sarr, akimiliki mpira dhidi ya David Kameta 'Duchu' katika mazoezi ya timu hiyo visiwani Zanzibar juzi. **PICHA: SIMBA**

## Mashujaa yataka wapya wanne, Geita Gold watano

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI ikiwa imebaki wiki moja kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa Januari 16, mwaka huu, benchi la ufundi la Klabu ya Mashujaa linatarajia kuongeza wachezaji wanne huku Geita Gold FC yenyewe ikisema inahitaji watano wapya ili kujiimarisha kwa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha wa Mashujaa FC, Hussein Bunu, alisema wanaendelea kufanya mazungumzo na wachezaji wanaowahitaji na kwamba mipango ikikamilika wataiweka hadharani.

"Tunatarajia kuongeza wachezaji wanne ambao tunaamini wataleta mapinduzi makubwa katika kikosi chetu ambacho mzunguko wa kwanza hatujapata matokeo mazuri," alisema Bunu. Alisema watasajili wachezaji wenye viwango na hawatasajili kwa ukubwa wa majina bali wataangalia wale wenye mafanikio.

Aliongeza kuwa leo asubuhi wataanza rasmi mazoezi baada ya kumaliza mapumziko ya muda mfupi, ili kuimarisha miili ya wachezaji huku wakisubiri ratiba ya Ligi Kuu kutoka.

"Leo tutaanza mazoezi kwa ajili ya kuwaweka sawa wachezaji malengo yetu ni kuendelea kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu ijayo," alisema.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Geita Gold, Denis Kitambi, alimwambia mwandishi wetu jana kuwa wanatarajia kuongeza wachezaji watano na tayari alishawasilisha mapendekezo ya aina ya wachezaji anaowahitaji hivyo anachosubiri ni utekelezaji tu.

"Nimetoa mapendekezo yangu, asubiri utekelezaji kwa kuwa malengo yangu ni kusajili wachezaji wenye kutoa ushindani," alisema Kitambi.

Kocha huyo alisema mapungufu aliyoyakuta wakati anakabidhiwa timu hiyo kwa sasa yanaendelea kuyapunguza siku hadi siku.

" Nataka kuitoa Geita Gold, ninaamini nitaifikisha mbali kutokana na ushirikiano ninaooneshwa na viongozi pamoja na wachezaji," alisema Kitambi.

Alisema mwishoni mwa wiki hii wanatarajia kuingia kambini moja kwa moja na kuanza maandalizi ya michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara mzunguko wa pili.

# *Banda awasili nchini kujiunga na Singida*

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa zamani wa Simba, Peter Banda, amewasili nchini tayari kujiunga na klabu yake mpya ya Singida Fountaine Gate.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo na vyanzo vingine zinasema raia huyo wa Malawi, aliwasili jana mchana kwa ajili ya kukamilisha taratibu za mwisho kabisa kujiunga na klabu hiyo katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufungwa Januari 15.

Habari zinasema kuwa Banda amesajiliwa kwa ada ya usajili wa Dola za Kimarekani 80,000, ambazo ni zaidi ya Sh. milioni 200 za Tanzania ambazo zitalipwa kwa awamu mbili.

Kwa sasa viongozi wa klabu hiyo wamekuwa wagumu kuzungumzia suala la usajili kwa sababu klabu hiyo imefungiwa kusajili na Shirikisho la Mpira wa Miguu Ulimwenguni (FIFA) pamoja na Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), mpaka hapo itakapokamilisha malipo ya aliyekuwa mchezaji wao, Rodrigo Carvalho.

Hata hivyo, chanzo chetu kimeeleza kuwa klabu hiyo imekuwa ikiingia mikataba na baadhi ya wachezaji wapya, na ipo katika hatua za mwisho kumlipa mchezaji huyo raia wa Brazil kabla ya kuruhusiwa kusajili, ndipo watakapowaingiza wachezaji wao wapya kwenye mfumo.

Mchezaji huyo mara ya mwisho aliichezea Big Bullets ya Malawi ambayo alijiunga nayo Agosti 29, mwaka jana, baada ya kuvunja mkataba na Klabu ya Simba kwa makubaliano ya pande zote mbili, huku mkataba wake na timu yake hiyo ukitarajiwa kumalizika Desemba 31, mwaka jana.

Banda alijiunga na Simba Agosti 2021, ambapo mkataba wake ulikuwa umalizike 2024, lakini ulivunjika kutokana na kutopata nafasi ya kucheza mara kwa mara, sababu kubwa ikiwa ni majeruhi.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE SAFI MADRID

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa na Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 25, amekubali dili la kujiunga na Real Madrid mwishoni mwa mkataba wake. (*Foot Mercato*)

### PHILLIPS AOTA MBAWA

KLABU ya Juventus imejiondoa kwenye mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Manchester City na England, Kalvin Phillips, kwa sababu ya ada ya mkopo na kiasi cha mshahara wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. (*Fabrizio Romano)*

### LIVER KUPATA FEDHA

LIVERPOOL wanaweza kupata kiasi kikubwa cha fedha kwa kiungo wa kati wa England, Jordan Henderson mwenye umri wa miaka 33 kama atauzwa na Al-Ettifaq ya Saudi Arabia. (*Mirror*)

### ONANA ALENGWA EVERTON

KLABU ya Everton imeweka ada ya pauni milioni 60 kwa Amadou Onana huku Arsenal wakilenga kumnunua kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 22. (*Football Insider*)

### TODIBO ATAJWA CHELSEA

CHELSEA, Manchester United na AC Milan zote zinamtazama mlinzi wa Nice na Ufaransa, Jean-Clair Todibo mwenye umri wa miaka 24, lakini Klabu hiyo ya Ufaransa inatumaini kuendelea kumshikilia katika dirisha la uhamisho la Januari. (*RMC Sport)*

### LINGARD ATAKIWA BARCA

BARCELONA imeripotiwa kupewa nafasi ya kumsajili kiungo wa zamani wa Manchester United na England, Jesse Lingard. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ni mchezaji huru tangu alipoondoka Nottingham Forest mwishoni mwa msimu uliopita. *(Sport)*

### TONEY HAJAKAMILISHA

MSHAMBULIAJI wa Kimataifa wa England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27, amesema "hajakamilisha biashara" anapojitayarisha kurejea Brentford baada ya kutumikia adhabu ya kusimamishwa kwa miezi nane kwa kukiuka sheria za kamari. *(Mirror*)

### MCKENNIE KUFUNGWA JUVE

KLABU ya Juventus iko tayari kufungua mazungumzo ya kuongeza mkataba na kiungo wa kati wa Marekani, Weston McKennie, 25. *(Goal)*


### AGUERD KUMPISHA KILMAN

KLABU ya West Ham itaangazia uwezekano wa kumnunua mlinzi wa Wolves, Max Kilman mwenye umri wa miaka 26, ikiwa mwezi huu watachangisha fedha kwa kumuuza mlinzi wa Morocco, Nayef Aguerd, 27. (*Guardian*)

### LONGSTAFF AWEKWA SOKONI

KIUNGO wa kati wa Newcastle United, Sean Longstaff, huenda akaondoka katika klabu hiyo ikiwa ofa sahihi itapatikana kwa Mwingereza huyo mwenye umri wa miaka 26. (*Sun*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG: KUNA WACHEZAJI HAWAMUDU PRESHA UNITED

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amependekeza baadhi ya wachezaji hawawezi kustahimili shinikizo la kuichezea Manchester United, lakini amesisitiza usajili kwa klabu hiyo bado ni "changamoto bora" kwa mwanasoka yeyote.

**Ten Hag ameidhinisha uhamisho wa mkopo wa Donny van Beek kwenda Eintracht Frankfurt katika dirisha la Januari huku Jadon Sancho akitarajiwa kurejea katika klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund kwa mkopo.**

Van de Beek alikuwa kwenye orodha ya walioteuliwa kuwania tuzo ya Ballon d'Or kabla ya uhamisho wake wa pauni milioni 35 kutoka Ajax mwaka 2020 na Sancho alikuwa mmoja wa wachezaji chipukizi wenye matarajio makubwa barani Ulaya alipowasili kwa mkataba wa pauni milioni 73 kutoka Dortmund mwaka 2021.

Hata hivyo, Ten Hag amesisitiza si mara zote klabu hufanya kosa wakati usajili wa hali ya juu.

"Hilo siku zote ni juu ya wachezaji hao na jinsi unavyojiamini katika uwezo wako, lakini naweza kukuambia jambo moja; Ligi ya England ni ngumu," alisema Ten Hag.

"Man United ni ngumu kuichezea kwa sababu ni rahisi kucheza karibu na timu nyingine yoyote, lakini kwa Man United kuna presha kubwa. Unapaswa kukabiliana na hilo.

"Lakini ikiwa unajiamini, hii ni changamoto bora na hakika hii ni klabu bora unayotaka kuwa kama mchezaji."

> Manchester ni ngumu kuichezea, ni rahisi kucheza timu nyingine, lakini ikiwa unajiamini...

Kushuka kwa kiwango cha Sancho tangu uhamisho wake kwenda Old Trafford miaka miwili na nusu iliyopita kumemfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 - kufukuzwa United kwa miezi minne kutokana na kutofautiana hadharani na Ten Hag na kupoteza nafasi yake kwenye kikosi cha England huku Van de Beek akiwa hajawahi kupata nafasi.

Van de Beek alicheza vema chini ya Ten Hag katika timu ambayo ilitinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019, lakini kocha huyo wa United alisema kuwa majeruhi kadhaa yalimaanisha kuwa hakuwahi kufikia kiwango sawa Old Trafford.

# ARSENAL BADO HAINA UHAKIKA KUSAJILI STRAIKA



**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesema "haionekani kama inawezekana" kwa Arsenal kusajili mshambuliaji Januari hii huku akikiri matatizo ya timu yake ya kufunga mabao yamekuwa tatizo la kisaikolojia.

'Washikabunduki' hao walitupwa nje ya Kombe la FA katika hatua ya raundi ya tatu Jumapili huku Liverpool ikishinda 2-0 kwenye Uwanja wa Emirates kwa mabao ya Jakub Kiwior na Luis Diaz.

Arsenal sasa wamefunga mara moja pekee kati ya mashuti 63 tangu Krismasi, na hivyo kuongeza shinikizo kwa klabu hiyo kumtaka mshambuliaji katika dirisha la usajili la Januari huku mchezaji wa Brentford, Ivan Toney akiwa ndio lengo lao kuu.

Lakini Brentford inathaminisha Toney kwa takriban pauni milioni 80 na wanasita kumuuza katikati ya msimu, na kumwacha Arteta akiwa kwenye wakati mgumu.

Arsenal sasa wameshinda mchezo mmoja tu kati ya saba iliyopita katika michuano yote ikiwa ni pamoja na kushindwa mara tatu mfululizo baada ya kufungwa na West Ham United na Fulham.

Alipoulizwa kama nafasi zao zilizopotea zimekuwa suala la kiakili, Arteta alijibu: "Labda imekuwa. Hasa baada ya leo (juzi) zaidi ya ilivyokuwa dhidi ya Fulham au West Ham kabla ya hapo.

"Ndio maana nadhani tunahitaji kuweka upya. Mapumziko haya ni mazuri. Yanakuja kwa wakati mzuri. Tutahisi pia jinsi tunavyohisi na jinsi ninavyohisi kuwahusu katika nyakati ngumu.

"Natumani naweza kuona hilo kutoka kwa watu wengine pia. Sasa mambo ni magumu, tuone wamesimama wapi."

Gabriel Jesus alikosa mchezo dhidi ya Liverpool kutokana na tatizo la goti, lakini Arteta anatarajia mshambuliaji huyo wa Brazil kuungana na wachezaji wenzake kwa kambi ya katikati ya msimu huko Dubai kabla ya mechi yao inayofuata dhidi ya Crystal Palace Januari 20.

Jesus alikosekana miezi mitatu msimu uliopita kutokana na tatizo la goti katika fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar.

# Mauricio ajibu kuhusu Henderson

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino alitoa maoni machache alipoulizwa kuhusu uwezekano wa Chelsea kutaka kumnunua kiungo wa kati kutoka Ligi Kuu ya Saudia, Jordan Henderson, baada ya timu yake kushinda 4-0 kweye FA dhidi ya Preston.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa England alizua utata alipoondoka Liverpool na kuelekea Mashariki ya Kati wakati wa majira ya joto na inasemekana hana furaha na maisha katika klabu mpya ya Al Ettifaq.

Henderson (33), amebakiza nafasi yake katika kikosi cha England cha kocha, Gareth Southgate licha ya kuhamia Saudi Arabia.


Alisema: "Hatukuzungumza kuhusu majina. Kwa sasa, hatuzungumzii kuhusu wachezaji.

"Nilimwona Behdad (Eghbali), akiwa na Paul (Winstanley) na Laurence (Stewart). Nadhani tutakuwa na mazungumzo. Hatukuzungumza kuhusu majina au wachezaji. Kwa sasa tunaangazia wachezaji kama Andrey Santos."

Henderson ni gwiji wa Anfield, akiwa nahodha wa Wekundu hao kwa mafanikio katika Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kombe la FA na Kombe la Carabao kabla ya kutumia muda wake wa miaka 12 kucheza pale Merseyside.



# Dorival Junior kocha mpya Brazil



**RIO DE JANEIRO,** Brazil

KOCHA Dorival Junior ameondoka katika Klabu ya Sao Paulo ya Brazil kuchukua mikoba ya kuinoa Timu ya Taifa ya Brazil, klabu hiyo ilisema katika taarifa yake.

"Ni utimilifu wa ndoto binafsi, ambayo iliwezekana tu kwa sababu nilipata kutambuliwa kwa kazi iliyofanywa kule Sao Paulo," Junior alisema katika taarifa iliyotolewa na Sao Paulo.

"Pia ningependa kuwashukuru mashabiki kwa upendo wao wote na sapoti yao."

Shirikisho la Soka la Brazil (CBF), halikuthibitisha uteuzi huo mara moja. Lakini chanzo cha CBF kiliiambia The Associated Press Ijumaa kwamba Junior angepokea ofa kuchukua nafasi ya Fernando Diniz aliyefutwa kazi.

Rais wa Sao Paulo, Julio Casares, alisema uteuzi wa Junior na CBF "ni ushahidi mwingine kwamba tuko kwenye njia sahihi."

Kocha huyo, ambaye alishinda taji la Copa Libertadores akiwa na Flamengo mwaka 2022, aliipeleka Sao Paulo kutwaa taji lao la kwanza la Kombe la Brazil mwaka jana.

"Namtakia Dorival mafanikio katika changamoto yake inayofuata," alisema Casares.

Rais wa CBF Ednaldo Rodrigues alimfuta kazi Diniz Ijumaa, akisema anataka "kuendeleza mchakato wa kuchagua kocha wa kudumu."

## HABARI MICHEZO

# GAMONDI ATOA SABABU KIPIGO YANGA KWA APR

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imekiri kuzidiwa na wapinzani wao APR ya Rwanda, huku ikisema imeumizwa mno kufungwa idadi hiyo ya mabao na kutolewa kwenye hatua ya robo fainali ya Kombe la Mapinduzi linaloendelea mjini Zanzibar.

Kwenye Uwanja wa New Amaan Sports Complex, mjini humo, Yanga ilipata kipigo kisichotarajiwa cha mabao 3-1 dhidi ya APR katika mechi ya hatua ya robo fainali juzi.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi, alisema wapinzani wao walikuwa bora zaidi kipindi cha pili ambapo waliingia na mbinu ya kuwaadhibu kupitia mianya waliyokuwa wanaiacha wakati wanakwenda kushambulia.

"Tulicheza vizuri kipindi cha kwanza, tumefanya makosa kipindi cha pili tumeadhibiwa kwa sababu tumefanya makosa mengi ambayo yamefanya tupoteze mechi," alisema kocha huyo.

Hata hivyo, alisema kukosekana kwa takriban wachezaji 14 wa kikosi hicho kumechangia kwa kiasi kikubwa kupoteza mechi hiyo na kutolewa.

"Lakini kila mmoja anajua kuwa hatukuwa na wachezaji tegemeo takriban 14, wanane wako katika vikosi mbalimbali kwenye timu za taifa, baadhi ni majeruhi, mchezaji kama Jonas Mkude alipewa ruhusa ya kwenda nyumbani kushughulikia matatizo yake, lakini kazi kubwa tuliyoifanya ni kuwatambulisha kwa kuwachezesha wachezaji wengi wa kikosi cha pili, tumepoteza Kombe la Mapinduzi, tunawapongeza wapinzani wetu," alisema Muargentina huyo.

Gamondi alisema alikuwa anaitumia pia michuano hiyo kama maandalizi ya Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la FA, akiangalia vile vile baadhi ya wachezaji ambao hawakupata nafasi mara kwa mara.


"Kwa sisi muhimu ni Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa na Kombe la FA. Michuano hii tumeichukulia kwa ajili ya maandalizi na kuangalia baadhi ya wachezaji ambao hawakuwa wanapata nafasi mara kwa mara," alisema kocha huyo.

Yalikuwa ni mabao ya Soulei Sanda, Mbaoma Victor na Saraf Eldin Shaiboub, huku la Yanga likifungwa na Jesus Moloko.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema kipigo hicho kimewaumiza viongozi, wanachama na mashabiki wa Yanga.

"Kufungwa na APR kumetuumiza kama Wanayanga, ila tunawapongeza sana APR walikuwa na mchezo mzuri hasa kipindi cha pili, sisi tulicheza kipindi cha kwanza, cha pili wakarudi bora zaidi wakapata ushindi ambao umewapeleka hatua ya nusu fainali, sisi Yanga safari yetu katika michuano ya Kombe la Mapinduzi mwaka 2024 imetamatika katika hatua ya robo fainali, haikuwa riziki yetu, wenzetu walikuwa bora sana," alisema Kamwe.

Msimu uliopita timu hiyo ilitokewa hatua ya makundi. APR sasa itacheza na Mlandege katika hatua ya nusu fainali baada ya timu hiyo kuitoa KVZ kwa mikwaju ya penalti 3-2, baada ya kutoka suluhu ndani ya dakika 90.




Winga wa Yanga, Jesus Moloko, akifurahia baada ya kuuzamisha mpira wavuni na kuiandikia timu yake bao la kuongoza kabla ya APR kugeuza kibao na kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 kwenye mechi ya hatua ya robo fainali ya Kombe la Mapinduzi iliyopigwa juzi usiku katika Uwanja wa New Amaan Sports Complex mjini Zanzibar. **MPIGAPICHA WETU**

## Saido kinara mabao ya penalti Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Klabu ya Simba, Saido Ntibazonkiza, anaongoza kwa kufunga mabao ya penalti hadi kufikia raundi ya 14 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa takwimu zetu na zile zilizotolewa jana na Bodi ya Ligi ni kwamba Saido ana mabao matatu aliyoyafunga kwa mikwaju ya penalti hadi sasa ambapo Ligi Kuu imesimama kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi na Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) zanazotarajiwa kufanyika Jumamosi ijayo nchini Ivory Coast.

Kitengo cha Takwimu za Dawati ya Michezo la Nipashe, zinaonesha kuwa penalti ya kwanza aliifunga Oktoba 5, mwaka jana, Simba ikicheza dhidi ya Prisons, Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, akiongoza timu yake kuifunga Prisons mabao 3-1, akakwamisha nyingine Desemba 15, mwaka jana, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam dhidi ya Kagera Sugar, Simba ikishinda 3-0 na Desemba 23 katika uwanja huo huo alifunga penalti, timu yake ikitoka sare ya mabao 2-2.

Wakati raia huyo wa Burundi akiwa na mabao matatu ya penalti, wachezaji wanaofuatia wote wamefunga bao moja moja, huku jumla ya mabao kwa njia hiyo ikiwa ni 14 na idadi ya wafungaji ni 12.

Wachezaji hao ni Fabrice Ngoyi na Derrick Mukombozi wote Namungo, Prince Dube wa Azam FC, Jean Baleke wa Simba, Pacome Zouzoua na Stephane Aziz Ki wote wa Yanga, Daniel Lyanga wa JKT Tanzania, Lucas Kikoti wa Coastal Union, Erick Okutu wa Tabora United, Obrey Chirwa wa Kagera Sugar na Jumanne El Fadhili wa Prisons.

## Salah aanika mapengo ya Stars AFCON

INATOKA UK 24

chotegemea, huu ndio ukweli na sote tumeona.

"Tunahitaji wachezaji wanaoweza kufanya kitu, nimefurahishwa na baadhi yao akiwamo Tshabalala (Mohamed Hussein) kurudi katika ubora wake, lakini sijafurahishwa pia na kiwango cha wengine," alisema Amrouche.

Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, alisema mchezo ulikuwa mzuri na kuwapa ushindani mkubwa kwa sababu ya ubora wa kikosi cha Misri, kinachoundwa na wachezaji bora.

Alisema mchezo ulikuwa kipimo kizuri na kumpa nafasi kocha kufanyia kazi mapungufu ya kikosi cha timu hiyo kabla ya kuanza kwa fainali za AFCON.

"Kocha ameona maeneo ya kufanyia marekebisho, atajaribu kuandaa timu kuona kiwango tulichokionesha leo (jana), maeneo tuliokuwa mazuri na nini kinatakiwa kuongeza na wapi kutumia makosa ya mpinzani ili kupata matokeo mazuri katika mechi yetu ijayo dhidi ya Morocco," alisema Samatta.

Stars itaanza kutupa karata yake ya kwanza kwenye fainali hizo Januari 17 dhidi ya Morocco na kisha Januari 21 dhidi ya Zambia kabla ya kumaliza mechi zake za hatua ya makundi Januari 24, mwaka huu dhidi ya DR Congo.

## Simba yafunguka ya Onana na JS Kabylie

INATOKA UK 24

kikosi chao na mchezaji huyo ataendelea kuwa sehemu ya kikosi cha timu hiyo kwa kipindi chote cha msimu huu hadi mwishoni wa mkataba wake.

"Kwa sasa Onana ni mali ya Simba hakuna ofa iliyofika mezani kwetu kutoka JS Kabylie, kwa sasa sio rahisi kumtoa mchezaji ambaye ameingia katika mfumo wa mwalimu, tunaongeza watu kuboresha timu yetu," alisema Ahmed.

Alisisitiza kuwa baada ya kutambulishwa kwa wachezaji wawili ambao tayari wamewasajili bado wanaendelea kushusha vifaa vipya walivyovisajili kipindi cha dirisha dogo ikiwa ni sehemu ya maboresho ya timu yao.



Alieleza kuna usajili unaendelea kufanyika na wanatarajia kutambulisha nyota wawili ndani ya wiki hii kulingana na mapendekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Abdelhak Benchikha.

# Michezo

Jumanne Januari 9, 2024

Nipashe




**Arsenal haina uhakika kusajili straika** UK. 22

**BAHATI TU...**



Mshambuliaji wa Misri, Mohamed Salah, akipiga penalti dhidi ya Taifa Stars, ambayo alikosa lakini mpira ukagonga mwamba na kumgonga kipa Aishi Manula mgongoni kabla ya kujaa wavuni. Katika mechi hiyo ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Cairo nchini humo juzi usiku, Misri ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Salah aanika mapengo ya Stars AFCON

## ●●● Amrouche aahidi kuyamaliza kabla ya kuivaa Morocco, amsifu Tshabalala, Samatta naye asema...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kikosi cha Timu ya Taifa ya Misri kikiongozwa na mshambuliaji wao nyota, Mohamed Salah, kuonesha uzoefu na uwezo wao mkubwa dhidi ya Taifa Stars, Kocha Mkuu wa timu hiyo ya Taifa ya Tanzania, Adel Amrouche, amesema bado ana kazi ya kufanya kwa wachezaji wake kuweza kucheza kwa uwiano mzuri kabla ya mchezo wao wa kwanza wa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) dhidi ya Morocco.

Misri ikiwa nyota wake walimwonesha Amrouche mapengo katika kikosi chake kabla ya kuelekea Morocco kwenye fainali hizo, baada ya kuichapa mabao 2-0 katika mchezo wa kirafiki uliopigwa Uwanja wa Cairo nchini humo juzi usiku.

Mahmoud Ahmed Ibrahim Hassan maarufu Trezeguet, ndiye aliyeanza kufungua milango ya Stars kwa kupachika bao la kwanza baada ya kupokea pasi murua kutoka kwa Salah anayeichezea Liverpool ya England.

Salah ambaye alihusika katika mabao yote mawili, alipiga mkwaju wa penalti iliyogonga mwamba na kisha kumgonga mgongoni kipa wa Stars, Aishi Manula, kabla ya mpira kuzama nyavuni. Kama si kumgonga Manula mgongoni, tayari Salah alikuwa amekosa penalti hiyo.

Stars tayari imewasili katika mji wa San-Pedro ambapo watacheza mechi ya kwanza ya makundi ya Fainali za AFCON zinazotarajiwa kuanza Januari 13 hadi Februari 11, mwaka huu nchini Ivory Coast na Taifa Stars imepangwa Kundi F pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Morocco na Zambia.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Stars, Amrouche alisema mechi ilikuwa nzuri na kipimo sahihi kwa timu yake, lakini hakufurahishwa na kiwango kilichooneshwa na baadhi ya wachezaji wake.

Alisema ameona makosa katika kikosi chake na atahakikisha anafanya kazi haraka ndani ya siku nane zilizosalia kabla ya kucheza mechi yao ya makundi ya fainali hizo dhidi ya Morocco.

"Ninajua kile tulichonacho, lazima tukubali na uhalisia, kuna baadhi ya wachezaji wamecheza chini ya kiwango, nili-

INAENDELEA UK 23

## Simba yafunguka ya Onana na JS Kabylie

**Na Saad Akida**

WAKATI jana ikimtambulisha mshambuliaji Ladack Chasambi kutoka Mtibwa Sugar kujiunga nao kwa mkataba wa miaka mitatu, Klabu ya Simba pia imefunguka kuhusu taarifa zinazomhusisha kiungo wao mshambuliaji, Willy Essomba Onana, kutakiwa na JS Kabylie ya Nigeria.

Katika taarifa ya klabu hiyo jana, ilieleza kuwa imefanikiwa kumsajili Chasambi kwa mkataba wa miaka mitatau na tayari amejiunga na wachezaji wenzake waliopo Zanzibar kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi.


Lakini pia kutokana na taarifa zilizozagaa kuwa Klabu ya JS Kabylie ya Algeria ipo katika mazungumzo na Simba kuhusu kuhitaji huduma Onana, uongozi wa miamba hiyo ya Mtaa wa Msimbazi jijini Dar es Salaam umesema, haujawahi kupokea ofa wala simu kuhusiana na suala hilo.

Taarifa hizo zilizagaa mitandaoni zikieleza kuwa JS Kabylie wameonesha nia ya kutaka kumsajili nyota huyo wa Simba kutoka Cameroon ili kwenda kuchukuwa nafasi ya Simon Msuva ambaye waliachana naye hivi karibuni.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema hajapokea taarifa zozote kutoka kwa viongozi wake kuhusu klabu hiyo kupeleka ofa ya kutaka huduma ya Onana.

Alisema kulingana na hali ilivyo kwa sasa hawawezi kumtoa mchezaji yeyote kipindi hiki kwani, wanaendelea kukijenga

INAENDELEA UK 23




GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >